# Nipashe

Jumatano Desemba 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580431

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



PROFESA MBILINYI, 1938 -2020

siasa

Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

MJUE GWIJI PROFESA MOHSEN FAKHRIZADEH

'Vimbwanga' wanawake kupeana kisogo uchaguzi

•Waulizana umejipanga, unatuachaje, we jiengue'

UKURASA 11

**LATRA** yadhibiti upandaji wa nauli msimu wa Krismasi

UKURASA 2



**MURUGENZI** TWAWEZA atajwa kimataifa kuhusu mageuzi ya kiutawala

UKURASA 4

# WhatsApp yadaiwa kutumika udanganyifu mitihani ufundi

UKURASA 2




Mkurugenzi Mkuu wa Takukkru Meja Jenerali Julius Mbungo

# Baba aachiwa kesi ubakaji binti yake

UKURASA 17

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**MSHTAKIWA KESI MAUAJI YA MAWAZO ADAI KUWA MGONJWA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza ...

**UKURASA WA 5**

**UMMY AWAONYA NEMC KUKWAMISHA WAWEKEZAJI**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy...

**UKURASA WA 19**

**BIDEN RASMI URAIS MAREKANI**

JOPO la wajumbe maalumu lenye nguvu ya kumchagua Rais wa Marekani, maarufu 'Electoral College'...


## Majaliwa, Lowassa wamlilia Subhash

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, YANGA RASMI KUKINUKISHA ZANZIBAR UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elia Kuandikwa, wakati alipofika Ikulu ya Zanzibar kwa ajili ya kujitambulisha pamoja na kumpa pongezi kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mkuu, uliopita mwaka huu. **PICHA: IKULU.**

# WhatsApp yadaiwa kutumika wizi mitihani

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kagera, inawashikilia watu 67 wakiwamo wanafunzi 59 wa vyuo viwili vya ufundi stadi (VETA), wakuu wa vyuo hivyo wawili na wakufunzi sita kwa tuhuma za kufanya udanganyifu katika Mtihani wa Taifa wa Elimu ya Ufundi na matumizi mabaya ya ofisi.

Akitoa taarifa hiyo jana mjini hapa, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, John Joseph, alisema mbali na kukamatwa kwa watu hao, taasisi hiyo pia imekamata simu za mkononi 66 zilizokuwa zikitumiwa na wanafunzi hao katika vyumba vya mitihani na za walimu waliokuwa wakifanya maswali na kuwatumia majibu wanafunzi.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU aliwataja wanaoshikiliwa kuwa ni wanafunzi 38 wa Chuo cha VETA Bukoba kilichoko katika Manispaa ya Bukoba, wakufunzi wao wawili ambao walikuwa wasimamizi wa mitihani, Francis Mwangosi na Ssenabulya Daud pamoja na Mkuu wa Chuo hicho, Buluhi Mitinje.

Aliwataja wengine kuwa ni wanafunzi 21 wa Chuo cha Ufundi Tuinuane VTC kilichoko Kijiji cha Kabale, Kata ya Karabagaine wilayani Bukoba Vijijini, wakufunzi wao wawili ambao ni Charles Byabachwezi na Verdiana Myaka, Mkuu wa Chuo hicho, Emmanuel Jonas na wakufunzi wawili wa Chuo cha VETA Bukoba, Evodius Kaiza na Aderick Anastaz ambao walikwenda kusimamia mitihani katika Chuo cha Tuinuane. Alisema watuhumiwa wa Chuo cha Tuinuane walikamatwa siku ya kwanza ya mtihani Desemba 7 mwaka huu na watuhumiwa wa VETA Bukoba walikamatwa siku ya mwisho ya mtihani Desemba 11 mwaka huu.

Alisema walimu kwa kushirikana na wanafunzi walitengeneza makundi mawili ya WhatsApp likiwamo la Chuo cha Tuinuane linaloitwa Kabale VTC na la VETA Bukoba linaloitwa Secret Magic ambayo yalitumika kutuma maswali na majibu.

"Wanafunzi hawa walikuwa na simu katika vyumba vya mitihani, maswali yaliyowashinda, wenye smart phone walikuwa wakipiga picha na kuwatumia walimu ambao walitafuta majibu na kuyatuma katika makundi hayo, lakini ambao hawakuwa na smart phone walitumia ujumbe wa kawaida (SMS)," alisema.

Mbali na kukamatwa kwa watuhumiwa na simu za mkononi, pia walikamata fedha taslimu Sh. 151,000 zikiwa katika Chuo cha Tuinuane ambazo inadaiwa zilichangwa na wanafunzi kwa ajili ya kuwapa wasimamizi.

Alisema kuwa upelelezi kuhusiana na tukio hilo, unaendelea na kuwa watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukakamilika.

# LATRA yadhibiti nauli msimu wa Krismasi

**Na Beatrice Shayo**

UPANDISHAJI wa nauli kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya umedhibitiwa, huku baadhi ya abiria wanaokwenda Mkoa wa Dodoma wakikosa usafiri huo jana.

Nipashe ilifika Stendi ya Mabasi Ubungo jijini Dar es Salaam kujionea hali ya usafiri na kushuhudia baadhi ya abiria wakilalama kuwapo kwa baadhi ya mabasi yalioongeza nauli, hasa ya kwenda Mkoa wa Arusha.

Walidai kuwa baadhi ya mabasi yamepandisha nauli ya kwenda katika mkoa huo wa kitalii kutoka Sh. 28,000 hadi Sh 33,000 na yaliyokuwa na nauli ya Sh. 31,000 imekuwa Sh. 33,000.

Hata hivyo, ufuatiliaji wa Nipashe ulibaini kuwa ofisini, tiketi za mabasi zilikuwa zinauzwa kwa bei iliyopangwa na mamlaka, lakini baadhi ya vishoka walikuwa wakiwalangua abiria kwa kuwauzia bei tofauti kwa kisingizio kwamba hakuna usafiri.

Nipashe ilizungumza na wakala wa kampuni ya mabasi yanayofanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Kagera, akibainisha kuwa kwa sasa hana nafasi ya kumpokea abiria kwa kuwa nafasi zimejaa hadi Desemba 24 mwaka huu.

"Kwa sasa usafiri umeshaanza kuwa mgumu kutokana na sikukuu, mabasi mengi yameshajaza hadi sikukuu, leo (jana) yenyewe mabasi ya kwenda Dodoma hakuna, yamejaa tangu asubuhi," alisema.

Abiria mmoja aliyejitambulisha kwa jina la John Erinest, alisema amekosa usafiri wa kwenda Dodoma na kujulishwa mabasi yalikuwa yameshajaza tangu asubuhi.

Alisema wamejulishwa watapatiwa mabasi mbadala ili kusafiri kuelekea mkoani Dodoma.

Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria, Maulid Ujingwa, alisema kuwa juzi walibaini kuwapo na tatizo la kupandishwa kwa nauli kwa baadhi ya mabasi na kulidhibiti mapema tatizo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na askari wa usalama barabarani.

Alisema kwa jana kulikuwa na tatizo la uhaba wa mabasi ya kwenda Mkoa wa Dodoma na kulazimika kutafuta magari mbadala ili kubeba abiria.

**TRC YAONGEZA MABEHEWA**

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, alisema msimu huu wa sikukuu abiria wameongezeka na shirika hivyo kuongeza mabehewa kuwa 15 kutoka mabehewa manane.

Alisema awali yalikuwa yanaondoka mabehewa manane na kufika Novemba waliongeza siku za safari kutoka siku nne kwa wiki na kufikia sita kwa wiki.

Alisema kuwa treni itakuwa inaondoka Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kuelekea Arusha na Jumanne, Alhamisi na Jumamosi inatoka Arusha kuelekea Dar es Salaam.

Alisema nauli kwa daraja la tatu ni Sh. 18,700, daraja la pili Sh. 26,700 na daraja la pili la kulala ni Sh 44,400.

# Wazazi wagoma kuzika mtoto kwa madai kafia polisi

**Na Richard Makore, MAGU**

FAMILIA ya marehemu Said Masoud, mkazi wa Kijiji cha Llungu Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, imegoma kuzika mwili wa kijana wao kwa takriban siku nane kwa madai amefariki akiwa mikononi mwa polisi katika Kituo cha Polisi Magu Mjini.

Akizungumza na Nipashe, mama wa marehemu, Pendo William, alisema mtoto wake alikamatwa Desemba 3, mwaka huu baada ya kuamshwa na mwenyekiti wa kijiji hicho, Mashauri Kafula, usiku kwa madai kwamba anatakiwa kwenda kulinda sungu sungu.

Alisema katika kijiji hicho walikamatwa vijana wanane kwa mtindo huo na kupelekwa polisi usiku katika kituo kikuu cha Wilaya ya Magu.

Alisema baada ya kukamatwa ndugu waliendelea kumpelekea chakula na kumkuta akiwa salama pamoja na wenzake saba.

Aliongeza kuwa mtoto wake mpaka anafariki Desemba 6, mwaka huu hakujua alikuwa anashtakiwa kwa kosa gani.

Kwa mujibu wa mama huyo, majibu waliyopewa na daktari baada uchunguzi, mwanawe alifariki baada ya kupata mshtuko na kupata majeraha mguuni na kichwani.

Aliongeza kuwa baada ya kumuona mwanawe alimkuta akiwa na majeraha mguuni na sehemu ya sikio kwa juu kama alichomwa na kitu chenye ncha kali.

Mama huyo alisema mwanawe ni wa pili kuzaliwa, na kwamba kaka yake naye alifariki dunia kwa ajali ya gari Desemba 7, mwaka 2014.

Alisema wao wamegoma kuzima na mwili uko Hospitali ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, kwa kuwa wakati akikamatwa alikuwa mzima hadi alipofariki Desemba 6, mwaka huu.

Baba mzazi wa Masoud, Saidi Haruna, akizungumza nyumbani kwake katika kijiji cha Ikungu, alisema hawawezi kuzika kwa kuwa marehemu wakati anakamatwa na polisi, hakuwa anaumwa.

Alisema alienda akiwa mzima, na kudai kuwa Polisi wamehusika na kifo hicho, huku akiomba uchunguzi huru kufanyika kubaini ukweli.

Haruna alisema yeye na mkewe walibahatika kupata watoto watatu, na kwamba wawili wameshafariki na kubakia mmoja.

Mmoja wa vijana waliokamatwa wakiwa na kijana huyo, Patric Jacob, alisema, siku ya tukio ya kifo hicho, walikisia akilia kwa sauti ya juu akiwa ofisi ya mpelelezi wa wilaya.

Alidai alisikia polisi wakisema kwamba Masoud alikuwa jeuri baada ya kuharibu bomba katika kituo hicho.

Jacob alisema siku hiyo mwenzao (Masoud) akichukuliwa na polisi na kusogeza gari jirani na ofisi ya mpelelezi, na tangu hapo hawakumuona tena.

"Sisi tumekuja kujua kama mwenzetu kafariki baada ya polisi kuanza kutuita majina na tukawauliza Masoud yupo wapi, lakini hawakutujibu," alisema.

Aliongeza kwamba siku ya kukamatwa waliamshwa usiku na mwenyekiti wa kijiji kwa madai kwamba wanatakiwa kwenda kulinda na kuwapeleka ofisi ya kijiji kabla ya kuwafungia ndani na kuita polisi.

"Huo ndio ukawa mwisho wa marehemu kwa sababu walipopelekwa wakiwa wanane na kwamba wamerudi wakiwa saba," alieleza.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema hajui kuwapo kwa tukio hilo, na kwamba atalifuatilia.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa na Lowassa wamlilia Subhash Patel



**Na Christina Mwakangale**

MFANYABIASHARA na Mwenyekiti Mtendaji wa Motisun Group, Subhash Patel (pichani), amefariki dunia huku viongozi mbalimbali wa kitaifa wakituma salamu za rambirambi.

Taarifa kutoka katika familia ya Patel zilieleza kuwa, mfanyabiashara huyo alifariki dunia jana akiwa nyumbani kwake akiendelea na matibabu na kwamba anatarajiwa kuzikwa kesho kwenye makaburi ya Wahindu yaliyoko Kijitonyama.

Kampuni ya Motisun inamiliki hoteli za White Sands, Pearl sun Hotel & Resorts na Sea Cliff, pia huzalisha vinywaji kadhaa na vifaa vya ujenzi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika salamu zake alisema: "Hayati Subhash, ana mchango wake kwenye sekta ya viwanda, alikuwa rafiki wa wote, mcheshi, ametoa msaada kwa maskini na matajiri na hakuwa mbaguzi.

"Ninatoa pole kwa wanafamilia, ndugu na wote walioguswa na msiba huu. Taifa limempoteza mmoja wa wazalendo wake. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina."

Majaliwa alisema anahuzunishwa na kifo cha mfanyabiashara huyo ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Kadhalika, Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, alisema ameshtushwa na kifo cha mfanyabiashara maarufu huyo.

Lowassa alisema hayo katika taarifa iliyotolewa na ofisi yake ikisema: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa sana taarifa za kifo cha rafiki na mzalendo halisi wa nchi hii Subash Patel.

"Nimefahamiana na Subhash kwa muda mrefu na ukaribu wangu na yeye ulitokana na moyo wake wa kulisaidia taifa hili na watu wake. Wakati nikiwa na majukumu serikalini nilishuhudia jinsi alivyosaidia miradi mingi vijijini, yenye nia ya kuwatoa Watanzania kwenye umaskini.

"Hakika taifa limempoteza mmoja wa wazalendo halisi. Natoa pole kwa familia pamoja na Watanzania kwa kifo cha Subhash," alisema Lowassa.

Taarifa ya TPSF jana kwenye mtandao wa twitter ilisema Patel atakumbukwa kwa mchango wake wa kukuza sekta binafsi nchini.

"Tumesikitishwa na taarifa za kifo cha Subhash Patel. Alikuwa mkurugenzi wa bodi ya TPSF, mwenyekiti wa CTI na kiongozi maarufu Tanzania katika jumuiya ya wafanyabiashara wa Afrika Mashariki. Mungu aipumzishe roho yake kwa amani. Amen."

Subhash Patel ni mwanzilishi na mwenyekiti wa kampuni za Motisun Group yenye matawi yake katika nchi za Zambia, Uganda na Msumbiji.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, Patel alianza biashara tangu akiwa mdogo akiuza duka la baba yake katika kijiji cha Msoga, wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Aliendelea kukuza biashara zake hadi ilipofika mwaka 1992 alipoanzisha kiwanda cha kutengeneza bidhaa za vyuma jijini Dar es Salaam.

Ndani ya miongo miwili alianzisha shirika lenye kampuni 15 ndani yake zilizomletea utajiri wa mamilioni ya dola aliyowekeza zaidi kwenye kampuni zake zenye viwanda.

Pia taarifa hiyo ilieleza viwanda hivyo ni pamoja vya chuma, uchimbaji wa madini, viwanda vya saruji, usindikaji wa vyakula, ujenzi na utengenezaji wa kebo.

DERM GROUP

NOTICE OF HOLIDAY SEASON CLOSURE

Derm Group wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices (except for Derm Elevators Ltd) will be closed during the festive season with effect from Friday 18th December 2020.

Business will resume on Monday 04th January 2021.

Our operations in Bagamoyo, Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Mwanza, Tanga, and Zanzibar shall not be affected by this closure.

Any inconveniences caused is highly regretted.

We would like to thank all our clients and business partners in general for their continued patronage of our services throughout the year 2020.




DERM ELECTRICS (T) LTD Electrical, HVAC, Security, ICT Co. Contractors

SKYLINE PROPERTIES LTD

COAST CONCRETE POLES LTD

Derm Elevators

DTsmart



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamzi wa Mazingira (NEMC), Dk.Samuel Gwamaka (kushoto), akimtambulisha wafanyakazi na menejimenti ya uongozi wa baraza hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, alipotembelea kwa mara ya kwanza ofisi za baraza hilo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshtakiwa wa kesi mauaji ya Mawazo adai kuwa mgonjwa

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza kusikiliza utetezi wa mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Geita, ambaye alikuwa mgombea ubunge Jimbo la Busanda mwaka 2015, Alphonce Mawazo, inayowakabili washtakiwa watano.

Wanaoshtakiwa katika shauri hilo namba 9 la mwaka 2019 ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45) na Kululinda Bwire (31), wote wakazi wa Katoro mkoani Geita.

Mshtakiwa wa kwanza Alfan Apolinary (57) akiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Yisambi Siwale, alidai Novemba 13 mwaka 2015 akiwa katika shughuli zake za machimbo ya dhahabu mgodi wa Mwazimba, afya yake haikuwa nzuri, hivyo aliamua kwenda Zahanati ya Segese na saa 11 jioni baada ya vipimo alionekana kuwa anasumbuliwa na homa ya matumbo, U.T.I na malaria hivyo kulazwa.

Apolinary aliendelea kudai kwamba Novemba 14 mwaka 2015, aliruhusiwa na daktari ambaye hakumfahamu jina lake na kurudi nyumbani kwake Katoro, huku akiwa na vidonge alivyokuwa akitumia na cheti cha matibabu.

Alidai siku iliyofuata akiwa nyumbani kwake, aligongewa mlango na alipotoka nje alikamatwa na askari polisi na kupelekwa Kituo cha Polisi Katoro, alituhumiwa kwa kesi ya mauaji ya Mawazo.

Baada ya Wakili wa Utetezi kumaliza kumwongoza mteja wake, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Javelin Rugaihuruza, alimhoji mshtakiwa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Kabla ya matatizo hayo ulikuwa unaishi wapi?

**Shahidi**: Nilikuwa naishi Katoro.

**Wakili:** Umepata faida gani uko kwenye machimbo ya dhahabu?

**Shahidi:** Ni kujenga nyumba moja.

**Wakili:** Je, una wake wangapi?

**Shahidi:** Nina mke mmoja.

Wakili: Una watoto wangapi?

**Shahidi:** Nina watoto wanne.

**Wakili:** Novemba 13 mwaka 2015 ulikuwa wapi?

**Shahidi:** Nilikuwa Mwazimba nachimba dhahabu.

**Wakili:** Kwa nini hukuleta mchimbaji ili akusaidie katika kesi hii kubwa?

**Shahidi:** Sijaleta mchimbaji hapa mahakamani.

**Wakili:** Ulitibiwa kwa bima au kwa keshi?

**Shahidi:** Nilitumia keshi.

**Wakili:** Risti ya matibabu na fedha ya matibabu iko wapi?

**Shahidi:** Sina.

**Wakili:** Mahakama itaaminije kama wewe ulikuwa mchimbaji wa dhahabu?

**Shahidi:** Sina kitu cha kuleta.

**Wakili:** Uliandika maelezo yako polisi lini?

**Shahidi:** Sikuandika maelezo polisi.

**Wakili:** Ulipigwa katika kituo cha polisi?

**Shahidi:** Sikupigwa polisi.

**Wakili:** Wakati unakamatwa ulikuwa na miaka mingapi?

**Shahidi:** Nilikuwa na miaka 52.

**Wakili:** Kwa sasa una miaka mingapi?

**Shahidi:** Kwa sasa nina miaka 57.

**Wakili:** Pale ulipokuwa unatibiwa ulilazwa wodi gani?

**Shahidi:** Nililazwa wodi ya wanaume.

Wakili: Ulipofika hospitalini ulikuwa unajitambua?

**Shahi:** Nilikuwa najitambua.

**Wakili:** Wakati unaumwa walichukuwa vipimo gani kwenye mwili wako?

**Shahidi:** Walichukuwa kinyesi na damu.

**Wakili:** Dripu zilikuwa ngapi?

**Shahidi:** Zilikuwa mbili.

**Wakili:** Mganga Mfawidhi alikuwa anaitwa nani?

**Shahidi:** Sijui jina lake?

**Wakili:** Kwenye kadi yako ya hospitali ipo namba?

**Shahidi:** Haipo namba.

**Wakili:** Tiketi za basi kutoka Segese hadi Katoro hizo tiketi unazo hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sina na sikuleta hapa mahakamani.

**Wakili:** Ni kina nani wamekutengenezea kesi hii?

**Shahidi:** Ni nyinyi waendesha mashtaka.

**Wakili:** Wakati unakamatwa kulikuwa na nini?

**Shahidi:** Kulikuwa na uchaguzi mdogo wa udiwani.

**Wakili:** Unafahamu Moko?

**Shahidi:** Ndiyo Moko nazifahamu.

**Wakili:** Wewe ni muumini wa dini gani?

**Shahidi:** Dini ya Kiislamu.

**Wakili:** Nesi aliyekupa dawa jina lake nani?

**Shahidi:** Simjui.

**Wakili:** Fedha ulizolipa ni kiasi gani?

**Shahidi:** Sijui.

**Wakili:** Kwa nini wakukamate kwenye kesi hii?

**Shahidi:** Kila mtu anakamatwa tu.

**Wakili:** Mashahidi ulikuwa unawafahamu?

**Shahidi:** Nilikuwa siwafahamu.

**Wakili:** Wewe umeshtakiwa kwa kesi gani?

**Shahidi:** Kesi ya mauaji.

Baada ya upande wa Jamhuri kumaliza, upande wa utetezi nao ulimhoji kama ifuatavyo:

**Wakili:** Gari ni la nani?

**Shahidi:** Ni la CCM.

**Wakili:** Ni nani aliyejaza kadi ya kliniki?

**Shahidi:** Ni daktari.

Naibu Msajili Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada, Frank Mahimbali, aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba leo kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine wa utetezi.

Washtakiwa jana walirejeshwa mahabusu kwa sababu kesi inayowakabili haina dhamana.

Akisoma hati ya mashtaka, Msaidizi wa Kumbukumbu Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Martina Nelei, alidai Novemba 14, mwaka 2015, katika Kijiji cha Rudete Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walimuua Mawazo.

# Mkurugenzi TWAWEZA mageuzi ya kiutawala

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa TWAWEZA, Aidan Eyakuze, ametajwa kuwa mmoja wa watu 50 wenye ushawishi ulimwenguni wanaohamasisha mageuzi ya kiutawala.

Eyakuze ni mmoja kati ya Waafrika watatu pekee kwenye orodha hiyo na mmoja kati ya 11 ambao hawako katika utumishi wa serikali.

Taasisi ya Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) inayoshughulika na utawala bora na Apolitical, zimemtambua Eyakuze kwenye orodha ya watu 50 wanaohamasisha maboresho na mageuzi ya kiutawala baada ya mapendekezo ya wataalamu, utafiti kufanywa kwa waliopendekezwa na baadaye mapendekezo hayo kupitiwa na taasisi ya WEF. Washiriki huchaguliwa kutokana na sifa mbalimbali za uongozi zikiwamo: Kuweka msisitizo kwenye matokeo, ubunifu na kufanya majaribio, pamoja na uhusiano na wadau kijamii, kitaifa na kimataifa.

Taarifa iliyotolewa na TWAWEZA kwa vyombo vya habari jana ilisema, Eyakuze alichaguliwa kama mmoja wa watetezi bingwa wa wananchi wa kawaida.

Orodha hiyo ina lengo la kuangazia wanasiasa, watumishi wa umma na wajasiriamali wanaoweka msukumo wa mabadiliko katika serikali ulimwenguni. Kabla ya janga la Covid-19, serikali zilikuwa zinatafuta namna ya kutumia fursa za ubunifu pamoja na kupunguza athari zake. Covid-19 imekuza changamoto hii, na kuongeza umuhimu wa serikali zote duniani kuwezesha mbinu mpya za kukabiliana na mtikisiko wa kijamii na kiuchumi.

'Apolitical' ni mtandao wa watumishi wa umma katika nchi zaidi ya 160. Jukwaa hilo ambalo limebuniwa na kufadhiliwa na serikali mbalimbali, huandaa hafla, mikutano ya wadau, mafunzo na makala kwa watumishi wa umma ambazo husaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.

Baraza hilo la mabadiliko ya utawala hukutanisha wataalamu kutoka upande wa wafanyabiashara na serikali ili kusukuma mageuzi ya kiutawala yanayochochea ubunifu na kukuza ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wake Eyakuze alisema: "Ni heshima kubwa kujumuishwa katika orodha hii ya wanamageuzi wa kiutawala. Inatia moyo sana kuona majina ya watumishi wa umma kutoka nchi mbalimbali ambao wanaamini kwamba serikali hufanya kazi vizuri pale inapokuwa wazi, bunifu na sikivu. Wananchi wanapokuwa na uhuru wa kujieleza, kuchangia mawazo bunifu na kufanya kazi kwa umoja, ndipo wanapojiletea maendeleo. Najivunia kuwa sehemu ya harakati za wabunifu wanaoshawishi utawala mpya unaowaheshimu na kuwajibika kwa wananchi."

# DPP: Sheria ya utakatishaji imesaidia kupaisha uchumi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, amesema Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006 imeisaidia nchi kuanza kukua kiuchumi.

Alisema hayo juzi, katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV baada ya kuulizwa swali kuwa kuna malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara kukosa raha na wengine kukimbia nchini, kutokana na wimbi la kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi kila anayeonekana ana fedha.

Mganga alisema wafanyabiashara wanaokimbia nchi kama kweli wapo ingawa hana ushahidi, ni wale ambao walikuwa wanafanya mambo kinyume cha inavyotakiwa. "Hii sheria ya utakatishaji, bahati mbaya au nzuri Tanzania siyo kisiwa, ni sheria ambayo inatumika kote duniani na kuifuatilia hii na imesaidia nchi kiuchumi kwa sababu mtu badala ya kulipa kodi zile fedha anazoficha anafanyia mambo mengine," alisema.

Mganga alisema kesi hizi maarufu ya utakatishaji watu wasiwe na wasiwasi nayo kwani ipo kwa mujibu wa sheria na ilitungwa na bunge, hivyo waliopewa jukumu la kuisimamia lazima waisimamie.

Alisema sheria na matamko ya kimataifa zinazuia utakatishaji kwa kuweka misingi, na nchi zote lazima zifuate katiba kuhakikisha zinakomesha watu kutakatisha fedha na madhara ya nchi kutokufuata huo utaratibu unawekewa vikwazo.

"Kila wakati nchi tumekuwa tukifanyiwa utafiti ambapo Tanzania ipo nchi za SADC ambako kuna chombo ambacho kimeundwa ambacho kinafanya utafiti kuangalia kama Tanzania inafuata kanuni na maelekezo ambayo yametolewa kimataifa kuzuia utakatishaji kwa kungalia kama sheria inafuatwa, watu wangapi wametiwa hatiani," alisema.

Alisema nchi ikifanyiwa utafiti na kukuta haifuati taratibu za kimataifa inawekewa vikwazo ambapo madhara yake nchi haiwezi kuwa na uwezo wa kutuma fedha nje au mtu kutoka nje kutuma fedha kwenye nchi yako.

"Kwa hiyo hata walio na ndugu zao nje watakuwapo lakini hawawezi kuwatumia fedha ndugu zao waliopo nchini na hata kuagiza bidhaa nje itakuwa shida sababu umewekewa vikwazo," alisema.

Mganga alisema ukiwekewa vikwazo kama hivyo kunakuwa na ugumu wa maisha kwa wananchi kwa sababu bidhaa ambayo haizalishwi nchini hamuwezi kuipata na kama mtataka kuipata mtawekewa masharti magumu ili muipate.

Sheria ya kuzuia utakatishaji wa fedha haramu ya mwaka 2006, inayataja matendo ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu.

Miongoni mwa makosa hayo ni jambo lolote linalohusisha uingizaji na usafirishaji wa dawa haramu chini ya sheria ambayo inahusika na dawa za kulevya; ugaidi, ikiwamo kufadhili vitendo vya kigaidi; usafirishaji haramu wa silaha; kuhusika katika vikundi vya uhalifu wa kupangwa na ulaghai; biashara haramu ya binadamu na usafirishaji wa wahamiaji haramu; utumikishwaji wa kingono, ikiwa ni pamoja na utumikishwaji wa kingono wa watoto; usafirishaji wa bidhaa haramu za wizi na bidhaa nyinginezo.

Misingi mingine ni vitendo vya rushwa; kughushi; unyang'anyi wa kutumia silaha; wizi; utekaji nyara, kumweka mtu kizuizini kinyume na sheria, kuchukua mateka; magendo; kujipatia fedha au mali kwa vitisho; kugushi nyaraka; uharamia; kujinufaisha na taarifa za ndani; usafirishaji haramu wa viungo vya binadamu na uwindaji haramu.

Kadhalika, ukwepaji wa kodi; uvuvi haramu; uchimbaji haramu wa madini; uhalifu wa mazingira au kosa lolote ambalo waziri amelitaja kupitia gazeti la serikali, ikiwa limefanyika ndani au nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake katika jitahada za kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, akizungumza katika mkutano wa tathmini ya kampeni za taasisi hiyo, za kupambana na rushwa ya ngono kwa wasichana na wanafunzi iitwayo 'safari salama bila rushwa ya ngono', iliyofanyika jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanafamilia watatu wafariki ajali ya gari

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MFANYABIASHARA Peter Lwalimiko (66) na familia yake ya watu wawili wamefariki dunia katika ajali ya gari wakitokea mkoani Mbeya kurejea Iringa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, aliwaambia waandishi wa habari jana, kuwa ajali hiyo ilitokea eneo la Changalawe Mjini Mafinga, Wilaya ya Mufindi juzi saa mbili usiku.

Alisema ajali hiyo ilihusisha gari aina ya Toyota Land Cruiser yenye namba za usajili T 852 AHE, mali ya Peter Lwalimiko, ambaye ni dereva.

Kamanda Bwire alisema, kati ya waliopoteza maisha ni pamoja na askari polisi, Linda Mhewa (28), akiwa na mtoto wake Drayden Kuambiana (10) na dereva ambaye ni kaka wa Linda.

Alisema mfanyabiashara huyo alikuwa akitokea Mkoa wa Mbeya, kurejea nyumbani Iringa na chanzo cha ajali hiyo ni gari lake kumshinda na kuligonga kwa nyuma gari lenye namba za usajili T229DFL /T101AGY aina ya Scania, lililokuwa limeharibika na kuegeshwa kando ya barabara kwa kuzingatia sheria zote za usalama barabarani kwa kuweka alama.

"Watu wawili, Elika Mwinami (62) na Devota Mhewa (16), mwanafunzi wa kidato cha pili, walijeruhiwa na kulazwa katika Hospitali ya Mafinga.

Kamanda Bwire, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa dereva wa gari dogo na kushindwa kuzingatia alama za usalama barabarani.

Kamanda Bwire aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani pia, kuchukua tahadhari wanapokuwa barabarani ili kuepuka ajali zinazozuilika.

# Ummy awaonya NEMC kukwamisha wawekezaji

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, ameliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) nchini, kutokuwa kikwazo katika utoaji wa vibali vya mazingira kwa wawekezaji katika kutekeleza miradi ya kimkakati.

Alitoa agizo hilo jana, alipozungumza na Menejimenti na Wafanyakazi wa NEMC baada ya kufanya ziara ya kikazi katika ofisi za baraza hilo, Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi yanayotolewa na wawekezaji ndani ya nchi juu ya utoaji wa vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ambavyo taratibu zake zinachukua muda mrefu na kusababisha ucheleweshwaji wa maendeleo katika nchi na kuleta usumbufu usio wa lazima kwa wawekezaji.

"Katika hili nimewaagiza NEMC kuharakisha mchakato wa kutoa vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa wakati. Hata hivyo nimebaini kwamba ucheleweshwaji wa vibali hivyo kwa kiasi kikubwa hausababishwi na NEMC bali changamoto kubwa iko kwa wale washauri elekezi ambao ndiyo wanafanya hizo tathmini za athari kwa mazingira.

"Kuna haja kuwasimamia washauri elekezi wa mazingira ambao siyo waaminifu. Katika kusimamia hilo tutahakikisha tunaunda kanuni mpya ambazo zitasimamia wataalamu hao," Ummy alisema.

Kuhusu biashara ya chuma chakavu, Ummy alitoa siku 14 kwa baraza kukutana na taasisi nyingine zinazohusika na biashara hiyo, ili kuwa na mwongozo bora wa kulinda miundombinu ya umma.

Alibainisha kuwa biashara ya vyuma chakavu imekuwa na matatizo makubwa na kusisitiza haja ya kutoa elimu kwa umma ili kutambua taratibu na mambo ya kuzingatia katika utoaji vibali vinavyotolewa kwa wakusanyaji, wahifadhi na wasafirishaji wa vyuma chakavu.

"Tutakuwa makini zaidi kuhakikisha biashara ya vyuma chakavu inasimamiwa kikamilifu, ili kufikia azma ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, hatutaki biashara hii kuhujumu miundombinu ya serikali, tutakuwa makini zaidi kuhakikisha vyuma chakavu having'olewi kutoka kwenye mataruma ya reli, alama za barabarani au madaraja," alisema.

Ummy pia aliuagiza uongozi wa NEMC kutumia zaidi Ofisi za Kanda za Baraza ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi badala ya kazi nyingi kufanyika Makao Makuu Dar es Salaam, akiagiza kuongezwa kwa wataalamu katika ofisi hizo, ili kurahisisha utendaji kazi.

Waziri huyo pia alisema ofisi yake itaendelea na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira nchini katika ngazi zote.

"Tumeainisha maeneo makubwa manne ambayo tutayafanyia kazi, ili kutunza mazingira. Maeneo hayo ni viwanda, migodi, ujenzi holela katika vyanzo vya maji pamoja na usimamizi madhubuti wa biashara ya vyuma chakavu."

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo viongozi Simiyu, Tabora kuhusu madiwani

NI jambo la kutia faraja kuona kwamba baadhi ya viongozi wa serikali ngazi ya mikoa wameanza kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya uvunjaji wa sheria, kanuni na miongozo vinavyofanywa na madiwani dhidi ya watumishi, wakuu wa idara na watendaji wa halmashauri.

Vitendo hivyo vya kuwaonea watumishi, wakuu wa idara na watendaji, vimekuwa vikichangia kwa kiasi kikubwa kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara, hivyo kuathiri shughuli za utendaji.

Kubwa ambalo limekuwa likifanywa na madiwani ni kufanya maamuzi ambayo yanaingilia madaraka ya mamlaka nyingine husan yanayohusiana na nidhamu.

Hatuwatetei watumishi wa halmashauri kwamba hawafanyi makosa, lakini kuna sheria, kanuni na miongozi inayoeleza wazi kuhusiana na namna ya kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Yamekuwapo malalamiko katika halmashauri nyingi kuhusiana na madiwani kufanya maamuzi mbalimbali kuhusiana na makosa ya kinidhamu yakiwamo kuwasimamisha, kufukuza na wakati mwingine kuwakataa watumishi na watendaji wasiendelee kufanya kazi katika halmashauri zao.

Jambo la kutia moyo ni kuwasikia viongozi wa mikoa ya Simiyu na Tabora wakitoa kauli zenye maelekezo ya kuwazuia madiwani kuacha kufanya hivyo, badala yake kuwasiliana na mamlaka husika.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amewataka madiwani wa halmashauri zote katika mkoa huo, kutokuwa chanzo cha migogoro kwenye maeneo yao, huku akipiga marufuku tabia ya kuazimia kuwafukuza watumishi bila sababu za msingi.

Amesema hatokuwa tayari kukubali madiwani wa halmashauri yoyote kukaa kikao na kuanza kuazimia kumfukuza mtumishi yeyote wa serikali awe mkurugenzi, mkuu wa idara au kitengo na badala yake watumie njia sahihi katika kufanya uamuzi huo.

Alitoa kauli hiyo, wakati wa kikao kazi kilichofanyika mjini Bariadi ambacho kiliwashirikisha madiwani wote wa mkoa mzima, viongozi wa wilaya na halmashauri wakiwamo watumishi wa serikali, viongozi wa dini, vyama vya siasa kwa lengo la kuelezea mwelekeo wa mkoa kwa miaka mitano ijayo.

Aliwaeleza madiwani hao kuwa na upendo kwa watumishi wao na kushirikiana nao kila wakati, na siyo kutumia nafasi yao kutaka kuwafukuza au kuwakataa wasifanye kazi kwenye halmashuari zao. Alisema kama wataona kuna mtumishi yeyote wa serikali utendaji kazi wake siyo mzuri, washauriane kwanza na ofisi yake kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa, ili kuona njia gani sahihi ya kumwajibisha mtumishi huyo.

Akiwaambia madiwani kuwa kama kuna jambo kwenye halmashuari uongozi wa mkoa upo, katibu tawala yupo, mkuu wa mkoa yupo, hivyo wawaambie na kama watashindwa, watapeleka TAMISEMI.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewataka madiwani kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo wakati wa usikilizaji wa mashauri ya kinidhani na uchukuaji wa hatua za kidhamu kwa watumishi wa umma, ili kuepuka kuzalisha migogoro katika maeneo yao.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Nzega, na kwamba pamoja na sheria kuwa wazi, uzoefu unaonyesha baadhi ya halmashauri katika mkoa huo kuna mamlaka za nidhamu zimekuwa zikivunja sheria kwa makusudi. Alisema kuna baadhi ya madiwani badala ya kuchukua hatua kwa watumishi wanaotuhumiwa, wamekuwa wakiwakataa.

Alisema kitendo cha kuwakataa watumishi siyo miongoni mwa adhabu zilizotajwa katika sheria na mwongozo kuhusu mashauri ya nidhamu na rufani kwa watumishi wa umma.

Tunawapongeza wakuu hao wa mikoa, na tunatarajia na wengine watafanya hivyo, ili kumaliza kabisa migongano hiyo inayokatisha taamaa watumishi kufanya kazi katika halmashauri zetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Madiwani na wabunge tekelezeni 'Hapa Kazi Tu'

BAADA ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, wabunge na madiwani kula kiapo na sasa Baraza la Mawaziri kukamilika ni wazi kuwa viongozi waliopewa dhamana wanazingatia kuwa wapigakura wanatarajia waanze kuona matunda.

Ndiyo muda wa kuwatumikia na si kusubiri ikikaribia uchaguzi, wanarejea majimboni, mitaani na kwenye kata na vizawadi kuomba kura.

Katika mitaa, vitongoji, vijiji, hadi majimboni kuna matatizo lukuki ya wananchi yanayohitaji ufumbuzi tena kwa gharama nafuu au nguvu kazi ya kujitolea, inayohitaji kuhamasishwa na mbunge au diwani.

Kwa mfano vijijini kuna huduma duni za kijamii hasa majisafi na salama, tiba kwenye zahanati, barabara na ukosefu wa vyoo shuleni.

Mengine ni pembejeo na maghala, umeme kwenye huduma muhimu hasa zahanati na vyote vinahitaji ufumbuzi wako diwani na mbunge, mkishirikiana na mawaziri.

Tumieni weledi, uzoefu na ujasiriamali kuibua mbinu za kuwapunguzia Watanzania umaskini, magonjwa na ujinga.

Uongozi ni kuonyesha njia na si vinginevyo, badala ya kusubiri wananchi wakuletee shida zao ofisini au nyumbani kwako kwa ambao hawana ofisi, ni vyema mkaanza kuwatembelea mitaani.

Kuna vitu ambavyo ni vya kukera siku zote hasa mijini na mara kadhaa najiuliza katika mitaa yenye mabalozi na madiwani inakuwaje kunakuwa na uchafu kupindukia tena wa kukera?

Siku zote kunakuwa na malalamiko yakielekezwa serikalini. Si kila huduma isubiriwe serikali kuu kuja kusimamia au mkoa, uliye kiongozi kwenye eneo lako ujiulize umebuni nini kutatua kero hizo?

Ubunifu rahisi na ujasiriamali usio na gharama unaweza kutatua kero za uchafu mtaani ambao umekithiri miji na majiji makubwa kama Dar es Salaam.

Dar es Salaam ni chafu na wakati mwingine watu wanajiuliza viongozi hawapo? Au wako wapo? Siku zote mliochaguliwa kumbukeni kiongozi ni mwongoza njia na mhamasishaji na hayo ndiyo mafanikio.

Huduma za kijamii na changamoto ndogondogo zinazoweza kutatuliwa na wananchi wenyewe mitaani kwa kushirikiana na viongozi kama madiwani.

Mfano upo uwezekano wa kila mtaa kuwa na eneo maalum la kuhifadhi taka kama si dampo dogo, likajengewa uzio na miundombinu kudhibiti na kuzuia takataka zisizagae.

Hata kila kaya ikachangisha mfano Sh. 5,000 ili kupatikana eneo hilo na kulijengea miundombinu.

Hivi sasa utaratibu wa kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, umepotea na baada ya kupuuzwa maeneo yamekithiri uchafu.

Takataka zilizokusanywa kandokando ya barabara au mitaani, mitaroni, zimejaa na kuanza kutoa harufu, lakini baadhi imeziba, viroba vya takataka hukaa hata miezi kadhaa huku zikioza bila kupelekwa dampo bila kujali kuwa hali hiyo inahatarisha afya za wakazi.

Huko huko mtaani kuna wajasiriamali wadogo wanaozalisha taka kila siku mfano msimu huu ni wa matunda mengi kuanzia mananasi, maembe na mtikiti yote hayo husababisha inzi.

Maganda yaliyomenywa yanatupwa ovyo barabarani, achilia mbali mabaki ya miwa, kokwa za embe ambazo haziozi.

Wajasiriamali hawa waliopo mitaani wapewe mwongozo na kutekeleza kwa kuweka vyombo vya kuhifadhia taka na yote hayo yanategemea nyie viongozi.

Kiongozi anayeishi mitaa hii au popote kwenye jimbo, anashuhudia uchafu, watu hawazingatii usafi aanze kuwajibika.

Kutokana na jiji hili kuwa na idadi kubwa ya watu, uzalishaji wa taka ni mkubwa kwa siku, hivyo viongozi wa kisiasa na watendaji washirikiane kusafisha mji.

Uchafu haupendezi machoni wala harufu chafu za vinyesi na maji taka mitaro hazifurahishi pua, hivyo viongozi mliochaguliwa na wananchi kwa utaratibu wa kisiasa, mnasubiriwa mtaani kuwatumikia na si vinginevyo.

Kumbukeni barabara za mitaa zimejengwa kwa lami himizeni watu kuzitunza kwa kufanya usafi mitaroni na pembezoni na pia kuzifagia.

Uongozi si lele mama ni kutatua matatizo na kero za wananchi na kuleta suluhu kwa wapigakura wenu, kama ambavyo juhudi zilivyoonyeshwa na viongozi hao kwenye kuomba udiwani, ubunge uenyeviti wa mitaa na kufanya kampeni mtaani, nyumba kwa nyumba vivyo hivyo rudini tena katika jamii mfanye kazi.

# Waziri ataka wakulima wa ngano kuchangamkia fursa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amewataka wakulima wa ngano kuchangamkia fursa ya zao hilo, linalohitajika katika viwanda kwa kujiunga katika ushirika ili kulizalisha kwa wingi badala ya viwanda kuagiza malighafi hiyo nje ya nchi.

Prof. Mkumbo alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea moja ya viwanda vya Said Salim Bakhresa kilichoko Buguruni na kujionea uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Waziri pia alikwenda katika kiwanda cha Knauf Gypsum Tanzania, Mkuranga mkoani Pwani kinachozalisha gypsum na unga wake na kuridhishwa na uwekezaji ambao umeanza miaka mitatu iliyopita.

"Wakulima wa ngano wanatakiwa kujiunga katika ushirika na siyo kufanya kilimo cha mtu mmoja mmoja. Mahitaji ya malighafi ya viwanda hivi yanatoka nje, hivyo iko fursa hapa kwa wakulima wa ndani," alisema.

Prof. Mkumbo alisema hawawezi kutosheleza eneo hilo kwa mkulima mmoja mmoja, hivyo lazima wajiunge ili waweze kukopesheka na taasisi za fedha na kuzalisha mazao bora yanayokubalika ndani na nje ya nchi.

"Nimefurahi mwekezaji ametamka hapa yuko tayari kushirikiana na wakulima, ili kuzalisha mazao haya. Tumesikia historia ya Bakhresa alianza uwekezaji mdogo na sasa anamiliki kampuni nyingi na huo ndio uwekezaji ambao Rais Magufuli anataka," alisema.

Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa kampuni ya Bakhresa Group, Hussein Sufian, alisema serikali imeonyesha nia ya dhati ya kuwekeza katika viwanda na wanaamini yaliyojadiliwa siku hiyo yanatasaidia kukuza uwekezaji uliopo na unaokuja.

Alisema Bakhresa ana kampuni 17 zinazozalisha bidhaa mbalimbali zinazouzwa ndani na nje ya nchi zikiwamo Kenya, Uganda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Malawi, China na Yemen.

Alimweleza Waziri kuwa kampuni hizo zinajiendesha bila hasara na kutaja moja ya matatizo wanayokumbana nayo ni ukatikaji wa umeme mara kwa mara.

Pia alisema anashukuru kwa sasa kuna mabadiliko makubwa kwa kuwa wanapata ushirikiano mkubwa kutoka taasisi za uthibiti na uwekezaji na kwamba misuguano iliyokuwapo awali imepungua.

Akiwa kiwanda cha Knauf, Mkuranga, Prof. Mkumbo aliwapongeza kwa uwekezaji huo ambao unazalisha ajira kwa wazawa na kutunza na kuheshimu utu wa Watanzania.

Naye Mkuu wa Wilaya wa Mkuranga, Filberto Sanga, alisema moja ya matatizo wanayopokea kutoka kwa wawekezaji ni ukatikaji wa umeme ambao unaweza kuchukua hadi saa moja.

Alisema wilaya hiyo kwa mkoa wa Pwani inaongoza kwa kuwa na viwanda vingi ambapo hadi sasa viko zaidi ya 90 miongoni vikiwamo vidogo, kati na vikubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Knauf, Ilse Boshoff, alisema wanazalisha gypsum, unga wa gypsum na 'metal profile'.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akikabidhiwa tuzo ya benki ya ndani ya nchi inayopendwa zaidi, katika hafla fupi ya tuzo za Tanzania Consumer Choice 2020 zilizofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: HISANI YA CRDB.**

# CRDB yang'ara tena tuzo za ubora

**Na mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeibuka na tuzo ya benki ya ndani ya nchi inayopendwa zaidi (Most Preferred Domestic Bank of the Year) katika tuzo za Tanzania Consumer Choice Awards kwa mwaka 2020.

Tuzo hiyo iliyotolewa mwishoni mwa wiki iliyopita, ikiwa ni siku chache tangu CRDB ilipoibuka kinara katika tuzo zinazotolewa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) kama taasisi ya fedha iliyoongoza kwa kuwasilisha taarifa ya fedha bora kwa mwaka 2018/19 kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Tuzo za Tanzania Consumer Choice ni tuzo zinazotolewa kila mwaka zikilenga kutambua ubora wa biashara mbalimbali kutokana na kura zinazopigwa na wateja wake.

Akipokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abudlmajid Nsekela, aliwashukuru wateja na Watanzania kwa ujumla kwa kuichagua benki hiyo kama benki yenye asili ya ndani ya nchi inayopendwa zaidi.

"Ushindi huu ni ishara tosha kuwa wateja wetu na Watanzania kwa ujumla wana imani kubwa na benki yao ya CRDB, hivyo hii kwetu sisi ni deni ambalo tunapaswa kuwalipa kwa imani hii kubwa waliyotupa. Ahadi yetu ni kuendelea kutoa huduma bora zinazoendana na mahitaji ya wateja ambayo yamekuwa yakibadilika kila uchao," alisema Nsekela.

Mgeni rasmi katika tuzo hizo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitaka sekta binafsi kuwa mstari wa mbele katika kusukuma mbele gurudumu la uchumi wa nchi kwa kuwa sasa hivi wameshaelewa maono na mtazamo wa serikali katika masuala ya kiuchumi.

"Wito wangu kwa wafanyabiashara ni kuhakikisha wanazalisha bidhaa na kutoa huduma ambazo zitakidhi mahitaji ya soko la ndani, lakini kushindana katika masoko ya nje na naamini uwezo huo tunao na sisi serikali tutaendelea kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara," alisema Kigahe.

# Serikali yaahidi kipaumbele sekta binafsi uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeahidi kuendelea kuipa kipaumbele sekta binafsi kwa kuhakikisha kila anayetaka kuwekeza anawekewa mazingira mazuri na kuachana na ukiritimba.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Profesa Riziki Shemdoe, wakati akizindua mfumo utakaowarahishia wafanyabiashara na wawekezaji kupata taarifa muhimu wanapotaka kuwekeza ndani na nje ya nchi.

Mfumo huo ambao pia utawawezesha wafanyabiashara kujua fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi umetengenezwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Nchini (CTI).

Akizungumza baada ya kuzindua mfumo huo, alisema serikali imejikita kwenye kuweka mazingira wezeshi, ili kila mwekezaji anayekuja achukue muda mfupi kupata anachotaka ili kuwavutia wengi zaidi kuja kuwekeza.

"Hata Rais John Magufuli wakati anazindua Bunge la 12 alisisitiza umuhimu wa kuondoa urasimu na kuhakikisha sekta binafsi inapewa kipaumbele na wanaokuja kuwekeza wanasaidiwa wasipate usumbufu wowote na hii inaonyesha namna gani serikali inavyoipenda sekta binafsi," alisema.

Profesa Mdoe alisema mfumo huo mpya utawasaidia wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje ya nchi na wa ndani kupata taarifa muhimu kwa urahisi wanapotaka kuwekeza tofauti na ilivyokuwa awali.

Aliishauri CTI kuutangaza mfumo huo ili wafanyabiashara wengi na wawekezaji wajue namna ya kuingia na kupata taarifa muhimu badala ya kuhangaika kwenda wizarani na kwenye taasisi za umma kutafuta taarifa za uwekezaji.

"Huu mfumo unapatikana dunia nzima utakuwa msaada mkubwa kwa wafanyabiashara kupata taarifa tunachotakiwa kufanya ni kuutangaza kwa nguvu kuhakikisha watu wengi wanaujua na wautumie kupata kile wanachotaka," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kuvutia uwekezaji zaidi kutoka ndani na nje ya nchi na kuhakikisha uhusiano mzuri uliopo baina ya sekta ya umma na binafsi unaendelea kuimarika ili kukuza mazingira ya baishara.

"Ukitaka kujua kwamba sekta binafsi na ya umma tuko vizuri ni huu mkutano kwa sababu walitualika na tumekuja kusikiliza changamoto zao na kutafuta suluhisho na waulize wenyewe wanasema namna tunavyoshirikiana vizuri," alisema Profesa Mdoe.

Paulo Makanza ambaye ni Mwenyekiti wa Kwanza wa (CTI), alisema waliamua kuanzisha mfumo huo kuwarahishia wafanyabiashara na watu wanaotaka kuwekeza kupata taarifa muhimu sehemu moja ya nini cha kufanya na hatua za kuchukua.

"Si watu wote wanajua wanatakiwa wafanye nini au wawe na kitu gani wanapotaka kuwekeza sasa mfumo huu utakuwa jibu kwao kwasababu wakiingia tu wataelimishwa hatua zote wanazotakiwa kuchukua zamani ilikuwa lazima uzunguke kwenye wizara na taasisi za umma," alisema Makanza.

# WMA yapata ufumbuzi udanganyifu madini

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Vipimo Tanzania (WMA), imenunua mashine za kupima na kuhakiki madini nchi nzima, hivyo kuwa na uhakika wa vipimo sahihi vya rasilimali hiyo.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Meneja wa WMA Mkoa wa Arusha, Dismas Maturini, wakati wa semina kwa wajasiriamali kuhusu umuhimu wa kuwa na vipimo sahihi.

Alisema WMA imekuwa ikipita nchi nzima kuangalia namna mashine hizo zinavyotumika ili kuhakikisha biashara hiyo inafanyika kwa njia halali ili wafanyabiashara wapate haki zao na serikali ipate haki yake.

Dismas pia alisema wamekuwa wakipima mita za maji kabla ya kuanza kutumika na kuweka lakiri maalum, ili kuhakikisha watumiaji wa maji wanapata bili za maji zilizo halali.

"Hizi mita zikihakikiwa zinawekewa alama maalum zinakuwa zimemhakikishia mtumiaji wa maji kwamba mita hiyo haiwezi kuchezewa na akipata bili anapata iliyohalali," alisema.

Alitoa wito kwa wajasiriamali wanaoagiza mita nje ya nchi kwenda WMA kabla ya kuagiza, ili waweze kuzipima na kuhakiki kama kweli zinasifa ya kutoa huduma hiyo kwa hapa nchini.

Meneja Mawasiliano wa WMA, Irene John, alisema wajibu mkubwa wa wakala ni kuhakikisha mlaji anapata vipimo sahihi na haibiwi na watu wanaopenda kutumia vipimo vya ujanja ujanja.

Alisema wakala katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro wameanza kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi.

Hivi karibuni, WMA ilitambulisha mizani mipya ya bei nafuu ambayo inatengenezwa na Watanzania ambayo wengi watamudu kuinunua kwa ajili ya shughuli zao za kibiashara.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema hivi karibuni mizani hiyo inatengenezwa kwa malighafi za Tanzania na ni rahisi kulinganisha na mizani kutoka nje ya nchi ambayo ilikuwa ikiagizwa kwa fedha za kigeni.

"Mizani hii imetengenezwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa ni rahisi na inapatikana kwa wingi sana kwa hiyo tunawaambia Watanzania wachangamkie bidhaa hizi zinazotengenezwa na wenzao maana zina ubora," alisema.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi huyo alisema Watanzania wametengeneza kipimio cha pampu ya petroli kwa ajili ya kuwahakikishia kipimo sahihi wanunuzi wa bidhaa za petroli wasipunjwe.

"Pampu za petroli zina kipimo chake maalum cha kupimia, ili muuzaji na mnunuzi wapate kipimo sahihi kama umenunua lita 20 basi ziwe ni lita 20 kweli kwa hiyo muuzaji lazima awe na hiko kipimo," alisema.



Mafundi wakiendelea na ujenzi katika kituo cha mabasi ya mwendo kasi eneo la Ubungo stendi ya mkoa, jijini Dar es Salaam. PICHA: MIRAJI MSALA

# TTCL kuboresha huduma sikukuu

Na Hellen Mwango

SHIRIKA la Simu Tanzania (TTCL), kupitia kampuni yake tanzu T-Pesa limedhamiria kuondoa malalamiko kwa wananchi kwa kuboresha huduma msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Biashara TTCL, Vedasto Mwita, alisema wananchi wanaotumia huduma za mtandao huo wamekuwa wakinung'unika na kulalamika kuhusu kasi kubwa matumizi ya vifurushi.

"Msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka tunahakikisha tunaondoa malalamiko yote kwa kuwa mteja akijiunga kifurushi cha wiki moja atakitumia mpaka huo muda utakapofikia kikomo, nyumbani kumenoga tumeamua kuboresha huduma kwa Watanzania watumie cha nyumbani kwa raha zao," alisema Mwita.

Naye Mkurugenzi wa T Pesa, Lulu Mkude, alisema ili kuhakikishia jamii kama kweli nyumbani kumenoga, huduma za T Pesa zinapatikana nchi nzima na wananchi wanafurahia kutumia cha kwao.

Alisema msimu huu sikukuu za mwisho wa mwaka kupitia bidhaa yao mpya ijulikanayo kama 'Tam Tam Plus' Watanzania watapata huduma mpya kupitia vifurushi vya Jisoti.

"Ofa hii maalumu watanufaika watumiaji wote wa T Pesa ikiwamo bando la intaneti, ujumbe mfupi pamoja na muda wa maongezi," alisema Mkude.

# RC akunwa utekelezaji wa miradi maendeleo

Na Mwandishi Wetu, IKUNGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, ameipongeza Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida kwa mapato na matumizi sahihi ya fedha za umma.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa Baraza jipya la Madiwani, alisema kwa mkoa huo halmashauri hiyo imekuwa ya mfano katika kukusanya na matumizi ya fedha miradi inayogusa maisha ya watu.

"Mmefanya kazi nzuri sana katika kukusanya, kusimamia matumizi ya fedha za umma, sasa nawataka mtekeleze ilani ya CCM ya sasa kwa kusaidiana na madiwani ili tuone matokeo makubwa zaidi kwa maisha ya wananchi," alisema.

Alimwagiza DED kuhakikisha ndani ya miaka mitano anaanzisha kiwanda cha ngozi kwa kuwa Ikungi kuna ng'ombe wengi pamoja na kuwa na shamba la ekari 2,000 za parachichi.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema Sh. milioni 280 kati ya Sh. milioni 670 ambayo ni asilimia 40 ya bajeti ya halmashauri, zilitolea katika nusu mwaka wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya afya na elimu huku Sh. milioni 81 zikitolewa kwenye vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Mpaka sasa Halmashauri ya Ikungi imekusanya Sh. bilioni 1.1 kwenye nusu hii ya mwaka 2020/2011 ambayo ni asilimia 54 ya makusanyo yote ya Sh. bilioni 1.92," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kazi nzuri ya kukusanya asilimia 54 ya mapato kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, mwaka huu, fedha ambazo zilitumika kwenye miradi ya maendeleo.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ally Mwanga, alimpongeza mkurugenzi huyo kwa kusimamia vizuri na kukusanya mapato katika kipindi ambacho madiwani walikuwa kwenye uchaguzi.

Aliwashukuru watendaji wa halmashauri hiyo kwa uaminifu katika kazi za kutumikia wananchi, huku akiahidi kufanyakazi kwa bidii katika kuiletea maendeleo halmashauri hiyo ambayo yanagusa maisha ya watu moja kwa moja. Aliwataka madiwani kutambua wajibu wao kama watumishi wa wananchi na kwamba ni muhimu kuunga nguvu, ili kuisimamia vyema halmashauri, kuhakikisha wanafanya vikao vya maendeleo ya kata (WDC), ili kuibua miradi ya kipaumbele.

Naye, DC Mpogolo aliwataka madiwani hao kusimamia mapato ya halmashauri na kuleta umoja miongoni mwao ikiwamo kukumbuka deni kubwa walilonalo kwa wananchi.

"Wasikilizeni wananchi, tatueni matatizo yao mkishirikiana na serikali, nitahakikisha nakuwa kiungo kizuri kati ya serikali kuu na halmashauri na kumsaidia mkurugenzi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi," alisema.

HABARI KITAIFA

## Sababu kuadimika mbegu za pamba

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKULIMA wa pamba wilayani Kishapu, Mkoa wa Shinyanga wamedaiwa kuuza mbegu za zao hilo, kwenye viwanda vya kuchakata mafuta ya kupikia, na kusababisha uhaba wa mbegu hizo.

Mkaguzi wa zao la pamba wilayani Kishapu, Thomas Tiluhongelwa, ambaye ni mwakilisha wa Bodi ya Pamba, alibainisha hayo juzi, wakati wa kuapishwa madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema hitaji la mbegu za pamba kwenye halmashauri hiyo katika msimu wa kilimo 2020-2021 zilikuwa ni kilo 1,000,000, lakini Bodi ya Pamba wakazidisha na kutoa kilo 1,300,000, lakini cha ajabu baadhi ya wakulima waliziuza kwenye viwanda vya mafuta, na kusababisha kuwapo tena na upungufu wa mbegu hizo.

"Malengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu katika msimu wa kilimo cha Pamba mwaka 2020-2021 ni kulima hekali 200,000, hivyo hitaji la mbegu likawa ni kilo 1,000,000, na sisi tukazidisha na kutoa kilo 1,300,000, lakini baadhi ya wakulima ambao siyo waaminifu wameziuza mbegu kwenye viwanda vya mafuta," alisema Tiluhongelwa.

"Sasa hivi kuna upungufu mkubwa wa malighafi kwenye viwanda cha kuchakata mafuta ya kupikia yatokanayo na pamba, kutokana na msimu wa kilimo uliopita (2019-2020) hapakuwa na pamba nyingi, hivyo kinachofanyika ni kutembelea wakulima na kuwarubuni kwa kuwauzia mbegu za pamba," aliongeza.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Shadrack Kengese, alilaani kitendo hicho, na kuwataka madiwani wa halmashauri hiyo wazuie tabia hiyo ya kuuza mbegu za pamba, pamoja na maofisa kilimo kwenda kutoa elimu kwa wakulima namna ya kulima kilimo chenye tija badala ya kulima kimazoea.

Naye Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, alisema wananchi wanapaswa kuhamasishwa kulima mazao ya chakula, ambayo yanastahimili ukame, kutokana na mvua za mwaka huu kutokuwa za kutosha.

# Madiwani wapewa kazi vyumba vya madarasa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, wametakiwa kwenda kufanya kazi ya kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Shadrack Kengese, alibainisha hayo wakati wa kuwaapishwa madiwani wa halmashauri hiyo, ambao walishinda kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Alisema jukumu la kwanza ambalo wanatakiwa kulifanya madiwani hao baada ya kula kiapo, ni kwenda kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, ili wanafunzi watakaoanza masomo Januari mwakani wasisomee chini ya miti na kukaa chini.

**Nitasimamia vizuri fedha za mapato ya halmashauri hiyo, pamoja na kudhibiti ubadhirifu, ili zikatekeleze shughuli mbalimbali za maendeleo.**

"Madiwani mmeshakula kiapo na kuwa madiwani rasmi, hivyo nawaomba jukumu la kwanza ambalo mnatakiwa kwenda kulifanya ni kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, ili wanafunzi wasikae chini na kusomea kwenye miti," alisema Kengese.

Mmoja wa madiwani hao, Edward Nkuba kutoka Kiloleli, alisema watakwenda kulifanyia kazi suala hilo la upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, kwa kushirikiana na wananchi pamoja na Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond.

Naye Mkurugenzi Mteandaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Jonsoni, aliwaomba madiwani kuwa na ushirikiano kwenye ujenzi wa miundombinu hiyo ya shule, ambapo tayari walikuwa wameshaanza ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye baadhi ya shule.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kishapu, William Jijimya, alisema atasimamia vizuri fedha za mapato ya halmashauri hiyo, pamoja na kudhibiti ubadhirifu, ili zikatekeleze shughuli mbalimbali za maendeleo, ikiwamo sekta ya afya na elimu.



Baadhi ya wanachama wa kikundi cha wakulima cha Jipe Moyo cha Kijiji cha Buanga, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakiangalia moja ya mizinga 11 ya nyuki waliokabidhiwa na Shirika la Swiss Contact juzi, ili kupanua wigo wa shughuli za kiuchumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wapigwa marufuku kukamata bodaboda usiku

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, amepiga marufuku polisi kufanya operesheni za usiku kwa kukamata madereva pikipiki zinazofanya biashara ya kubeba abiria kwa kisingizio cha ukaguzi wa leseni.

Aidha, amepiga marufuku askari wa usalama barabarani kukamata vyombo vya moto.

Mtatiro alitoa tamko hilo juzi, alipokuwa akizungumza na wadau wa usafirishaji wa pikipiki na bajaji, na kwamba amechukua hatua hiyo kufuatia operesheni iliyofanyika usiku wa kuamkia Desemba 14, mwaka huu, ambapo baada ya kupokea malalamiko ya unyanyasaji huo, aliendа polisi saa 7:15 usiku na kuwatoa madereva pikipiki 24.

Mtatiro ambaye alionekana kukerwa na kutokana na kukerwa na tukio hilo, alimtaka Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) na timu yake kukaa, kujipanga na kutengeneza utaratibu wa kutoa elimu kwa madereva hao na kuwatafutia leseni kwa ghalama isiyozidi shilingi 70,000 katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwakani, ili kuondokana na kero za kusumbuana na madereva wasiokuwa na leseni.

"Mimi kama mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wa wilaya, nataka kuona operesheni za polisi zenye weledi zinazoenda sambamba na utoaji wa elimu ya usalama barabarani, ili kupunguza kero zisizokuwa za lazima kwa wananchi," alisema na kuongeza.

"Operesheni za Krismasi na Mwaka Mpya naziona zina walakini katika macho ya jamii, kwa vile zinaonyesha kulenga kujipatia kipato cha ziada na kujinufaisha."

Alisema hata utaratibu wa kuwakamata na kuwaweka ndani kwa kosa linalohitaji madereva wa vyombo vya moto kulipa faini huku magari na pikipiki vikiwa chini ya uangalizi wao bado pia ni uonevu, ambao unalenga kuigombanisha serikali na wananchi wake.

Awali wakizungumza kwa nyakati tofauti madereva hao, Omari Said Issa, Nyenje Ally, Mussa Mustafa Waziri, Omari Kadagaa na Hemedi Kandita, waliwatuhumu polisi kuwakamata bila makosa na kuwafanyia vitendo vya unyanyasaji vikiwamo kuwarusha kichura, kuwapiga, kuwaweka ndani na kuwapeleka mahakamani hata baadhi ya ndugu ambao wakati mwingine huenda polisi kwa ajili ya kufuatilia matatizo ya ndugu zao.

# Madiwani watakiwa kuzingatia sheria kuwajibisha watumishi

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

MADIWANI wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo wakati wa usikilizaji wa mashauri ya kinidhani na uchukuaji wa hatua za kidhamu kwa watumishi wa umma, ili kuepuka kuzalisha migogoro katika maeneo yao.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati wa uzinduzi wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji Nzega.

**Kwa sasa umetokea mtindo kwa wananchi kuvamia maeneo ya taasisi hizo na kusababisha migogoro.**

"Pamoja na sheria kuwa wazi, uzoefu unaonyesha kuwa baadhi ya halmashauri katika mkoa wetu kuna mamlaka za nidhamu zimekuwa zikivunja sheria kwa makusudi...chukueni hatua za kinidhamu bila kumwonea wala kumpendelea mtu," alisema.

Alisema kuna baadhi ya madiwani badala ya kuchukua hatua kwa watumishi wanaotuhumiwa, wamekuwa wakiwakataa.

Dk. Sengati alisema kitendo cha kuwakataa watumishi siyo miongoni mwa adhabu zilizotajwa katika sheria na mwongozo kuhusu mashauri ya nidhamu na rufani kwa watumishi wa umma.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Mkoa alitoa wito kwa madiwani, wakurugenzi, watendaji pamoja na menejimenti kuhakikisha kwamba maeneo yote ya taasisi za umma yanalindwa na kupimwa na kuwekewa mipaka.

Alisema kwa sasa umetokea mtindo kwa wananchi kuvamia maeneo ya taasisi hizo na kusababisha migogoro.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akipata maelezo ya utekelezaji wa mradi wa maji Mkuranga – Vikindu kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar-es-Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo. Mradi unatekelezwa na DAWASA na unatarajiwa kukamilika Februari, 2021 na utahudumia wakazi takribani 25,500. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miche ya michikichi milioni 5 kuzalishwa

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na wadau ikiwamo Jeshi la kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Magereza na Halmashauri sita katika Mkoa wa Kigoma, wameanza uzalishaji wa miche ya michikichi milioni tano kila mwaka kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ili kupunguza gharama za serikali kutumia fedha nyingi kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Akizungumza baada ya kutembelea mashamba makubwa ya uzalishaji wa miche ya michikichi ya Majeshi hayo ya Bulombola na Kwitanga, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk Geofrey Mkamilo, alisema uzalishaji huo umelenga kufikia miche ya michikichi milioni 20 katika kipindi cha miaka minne ijayo ambayo itaweza kuzalisha mafuta ya kula kila mwaka.

Alisema lengo la TARI ndani ya miaka mitano miche milioni 20 ambayo itaweza kupanda jumla ya hekta 160,000 ambazo zitaweza kuzalisha mafuta tani 720,000 kwa kipindi cha miaka minne ijayo na kuvuka mahitaji ya mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya tani 570,000.

"TARI kwa kushirikiana na taasisi nyingine tumedhamiria kumaliza hili tatizo la uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi... mafuta yanayoagizwa nje yanatokana na michikichi sasa tumeamua kuzalisha miche hiyo aina ya tenera ili kutoa mafuta ya kutosha na ndani ya miaka mine ijayo tatizo hili litakwisha," alisema Dk Mkamilo.

Dk Mkamilo,alisema kuwa mpaka sasa TARI kwa kushirikiana na Taasisi hizo wameshazalisha miche milioni 4.2 na hadi kufikiaa mwisho mwa mwaka huu miche milioni 5 itakamilika ambayo baadhi yao taasisi hizo zimeshapanda na mingine wakulima wamepatiwa bure ili kupanda mashamba yao.

Kwa upande wao kwa nyakati tofauti viongozi wa JKT Bulombola Kikosi cha 821 na Jeshi la Magereza Kwitanga ambayo yameitikia wito wa kulima kilimo cha zao la michikichi,yamewataka vijana kuachana na tabia ya kukaa vijiweni, badala yake kuchangamkia fursa iliyotolewa na serikali ya kilimo cha zao hilo.

Meneja wa Shamba la kikosi hicho,Meja Godfrey Mwakabole, alisema serikali imetoa fursa ya kilimo hicho kwa kuzalisha mbegu bora za kisasa na kuzigawa bure lakini bado vijana wameshindwa kuchangamkia na badala yake wanalalamika maisha magumu.

# Wilaya yaweka bei elekezi saruji

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

SERIKALI wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, imesema bei elekezi ya saruji ni Sh. 14,500 kwa mfuko mmoja, na kwamba mfanyabiashara yeyote atakayekiuka maelekezo hayo atakamatwa na kushtakiwa.

Maelekezo hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, wakati akizungumza na wadau na wananchi wenye mkutano wa wadau wa usafirishaji miji hapa, na kwamba hali hiyo imetokana na serikali kubaini uwapo wa wimbi kubwa la wafanyabiashara wa bidhaa hiyo kupandisha bei kiholela.

Mtatiro alisema katika wilaya yake wapo wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiuza bidhaa hiyo kati ya Sh. 15,000 hadi Sh. 18,000 kwa mfuko mmoja, na kwamba ameanza kuwakamata na wote watafunguliwa kesi za uhujumu uchumi.

Alisema wapo wafanyabiashara ambao walikuwa wanatumia vibaya na kujinufaisha kutokana na kufungwa kwa kiwanda cha Dangote kwa ajili ya ukarabati, na kwamba taarifa alizonazo ni kwamba hivi sasa kiwanda hicho kimeanza uzalishaji hivyo siku chache zijazo upungufu wa saruji uliopo utakwisha.

Kufutia hali hiyo, Mtatiro alitoa namba zake za simu na za katibu tawala wa wilaya hiyo kwa wananchi, ili kupiga au kutuma ujumbe wa kumweleza duka au jina la mfanyabiashara atakayeuza bidhaa hiyo kwa bei ya juu zaidi ya shilingi 14,500 kwa mfuko mmoja.

Alisema serikali haiwezi kuona au kuendelea kuvumilia na kufumbia macho vitendo vya baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kujinufaisha kwa kuwauzia wananchi saruji kwa bei za juu kwa nia ya kujinufaisha kwa kujipatia faida kubwa.

**Serikali haiwezi kuona au kuendelea kuvumilia na kufumbia macho vitendo vya baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kujinufaisha kwa kuwauzia wananchi saruji kwa bei za juu kwa nia ya kujinufaisha kwa kujipatia faida kubwa.**

## PROFESA MBILINYI, 1938 -2020



Ukurasa 13



Ukurasa 14

## MJUE GWIJI PROFESA MOHSEN FAKHRIZADEH

siasa
JUMATANO DESEMBA 16, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# 'Vimbwanga' wanawake kupeana kisogo uchaguzi

•'Waulizana umejipangaje, unatuachaje, we jiengue'

**Na Sabato Kasika**

VIROJA vya wanawake kwenye uchaguzi mkuu uliopita, vinaibua upya dhana kuwa hawapendani. Ni kutokana na madai kuwa walifanyiana 'figisu' katika mchakato wa kura za maoni za uchaguzi wa Oktoba 2020.

Lakini hata hivyo, hawakati tamaa wanasema licha ya kuwapo kasoro na dosari ndogo wana nafasi na watajitahidi kuzirekebisha.

Licha ya kwamba dhana kuwa wanawake hawapendani, haipewi nafasi na kinamama wanaharakati wanaopiga vita kwa nguvu zote wakiamini kuwa haina nafasi tena, ni suala linalotoa wakati wa kuitafakari na kuipatia ufumbuzi.

Wanaharakati wanaamini kuwa wengi wanashirikiana kwa mambo mengi, kama kutafuta uongozi ukiwamo wa kisiasa kama udiwani, ubunge na urais kwa kuwaunga mkono wenzao wajitokeza kuwania nafasi hizo, bila kujali tofauti za kiitikadi za kisiasa.

Pamoja na jitihada hizo za kuwafanya wapendane, inaelezwa kuwa wana safari ndefu kuachana na mtindo huo wa 'kupeana kisogo', kwa madai kwamba baadhi yao hawajabadilika.

Hayo yanawekwa wazi na baadhi ya wanawake waliojitokeza kuwania udiwani na ubunge katika uchaguzi wa mwaka huu, wakidai kwamba wenzao walikuwa mstari wa mbele kuwabagua.

Katika semina ya hivi karibuni ya kujadili siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ilioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Dar es Salaam, baadhi yao wanataja yaliyowakuta.

### KUULIZWA UMEJIPANGAJE?

Neema Mwinyimvua, aliyejitosa udiwani kata ya Mabibo Dar es Salaam, anadai alikwamishwa na wanawake wenzake waliomuuliza maswali yaliyoashiria kutaka kitu kidogo.

"Unalizwa umejipangaje, utatuachaje. Maswali kama hayo yaliashiria niwape chochote ili wanipitishe niwanie udiwani."

Neema anasema kuulizwa maswali hayo kulionyesha wanawake hawapendani na kwamba, kinachowekwa mbele zaidi ni kitu kingine si kuunga juhudi na kufanikisha ushindi.

"Umefika wakati wanawake tusiendelee kukumbatia dhana hii kwamba hatupendani na kumbe ni wenzetu wachache, ambao hawajaamua kubadilika na kuendekeza yale yanayozidi kututengenisha," anasema.

Mgombea huyo anasema, uhamasishaji ambao umefanywa na wadau wa kutetea haki za wanawake wakiwamo TGNP wa kuondoa dhana ya kutopendana umebadilisha wengi na kwamba waliobaki wafikiwe.

Mgombea mwingine wa udiwani kata ya Makurumla, Mpegwa Mhembano, anasema, wanawake waliokuwa miongoni mwa wajumbe, walimtaka aondoe jina katika kinyang'anyiro.

Sababu za kumtaka aondoe jina ni kuwa tayari kulikuwa na mgombea aliyekuwa ameandaliwa, hivyo asijusumbue kwani hawezi kupitishwa.

"Sikuondoa jina langu nikaingia hadi nikashindwa huko mbele. Lakini nilijifunza kwamba bado wanawake wanahitaji kuelimishwa kujua umuhimu wa kuungana," anasema Mpegwa.

Anasema, wanawake wanahimizwa kuungana, ili kusaidiana kuingia kwenye vyombo vya maamuzi, lakini kuna kumwamishana, hali ambayo itachangia kuwafanya waendelee kubaki nyuma.

"Ni kweli tunapendana, lakini niseme tu kwamba wapo wenzetu wachache wanatuharibia mshikamano huu wa kupambana na mfumo dume ili nasi tuwe wengi katika uongozi," anasema.

### HAKUNA KUKATA TAMAA

Vivian Ugulumu, anasema, alijitosa kuwania ubunge Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam akakosa kuungwa mkono na wanawake wenzake.

"Nilikwenda kwa wanawake wenzangu ndani ya chama na kuwaomba waniunge mkono kwa hali na mali, ili nifanikishe lengo langu la kuingia bungeni, lakini wengi wao walikataa kwamba hawana nafasi," anasema Vivian.

Anaeleza kuwa wakati umefika wanawake kuachana na mazoea kuwa wanaume ndiyo wanafaa kuongoza au kudhani kwamba ili mtu apate uongozi ni lazima awape chochote wajumbe ama wapigakura.

"Binafsi sijakata tamaa, panapo majaliwa nitapanda tena ulingoni katika uchaguzi wa mwaka 2025, kwa hiyo mapambano bado yanaendelea ya kutaka kuwatumikia wanawake wenzangu na Watanzania kwa ujumla," anasema.

Hata hivyo, mwanamama mwingine Theresia Luhanjala, anawapa somo waliojitosa udiwani na ubunge kwamba, waanze kuonyesha nguvu ya uongozi tangu ngazi za chini kwenye jamii ili wajulikane kwanza.

Theresia anasema, hatua hiyo inamfanya mtu kujulikana mapema ili anapojitokeza kuwania uongozi tayari watu wanamfahamu na hivyo kupata nafasi kwa urahisi kuliko kuhangaika na kuambulia patupu inaanzia chini.

"Mabadaliko yaanze na wewe kwa jirani yako, wezesha watu, hiyo itakusaidia kujulikana mapema, siyo katika mikutano ya hadhara ndipo unajitokeza wakati jamii haikujui vizuri," anasema Theresia.



Vivian Ugulumu, aliwania ubunge wa vitimaalum akitoa ya moyoni. PICHA : SABATO KASIKA

### DHANA HII ISIENDEKEZWE

Inaelezwa kuwa dhana kwamba wanawake hawapendani, imeshapitwa na wakati na haitakiwi kupewa nafasi, badala yake juhudi ziendelee kufanyika za kuelimisha wachache ambao hawajaona umuhimu wa kuwa pamoja.

Ofisa Programu ya Ujenzi wa Nguvu za Pamoja wa (TGNP), Anna Sangai, mwezeshaji katika semina hiyo, anasema, wanawake wamesimama imara kuunga mkono wenzao wanajitokeza kutafuta uongozi.

"Wanawake wanapendana na wana uwezo wa kuongoza, hivyo wachache wasitukatishe tamaa, tuendelee kusonga mbele katika juhudi za kutetea haki za wanawake na kusaidiana kupata nafasi za uongozi," anasema Sangai.

Ofisa huyo anasema, kwa sasa imebaki dhana ni kuwa wanawake hawapendani, na kwamba haina uzito, hivyo wanawake wasiendelee kuishi kwa kuzingatia dhana hiyo ambayo kwa sasa imepitwa na wakati.

# MKWAMO BUNGE, CHADEMA

## •Kiini kilichoko mkanganyiko sheria
## •Suluhu ni katiba mpya, mikataba AU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MVUTANO unaoendelea kuhusu uhalali wa wabunge wanawake wa viti maalum kutoka CHADEMA unaingia mwezi mwingine ukiwaacha wananchi na maswali yasiyojibiwa, huku kila upande ukitumia sheria, miongozo na katiba kuthibitisha uhalali wa kile kilichoamuliwa.

Licha ya wengi kudhani kuwa mkwamo unaweza kumalizika kwa kuruhusu wagombea binafsi au huru watakaoingia bungeni bila kuteuliwa au kushindana kupitia vyama, kuna mengi ya kuangalia kabla ya kufanya maamuzi.

Kugombea binafsi kunaweza kuwa jukwaa la kuwafikisha wabunge wa kambi rasmi ya upinzani bungeni, ambao hawatakuwa na vikwazo wala kutishiwa kuenguliwa uanachama na yeyote.

Kuwa na wagombea huru ndiko kunakodhaniwa kuwa kutamaliza misuguano ya muda mrefu ya wabunge kufukuzwa bungeni kwa madai kuwa chama hakina imani nao na wakati mwingine wabunge kuonyesha misimamo inayopingana na ya wakuu wao au itikadi za vyama.

Lakini, ibara ya 67(1) ya katiba ya Tanzania inazitaja sifa za kuteuliwa kuwa mgombea ubunge kuwa ni pamoja na kuwa mwanachama wa chama cha siasa na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kisheria.

Aidha, sifa za kuteuliwa kuwa mgombea urais ni nyingi, lakini kubwa ni lazima mgombea atokane na chama na chama ndicho kinachompendekeza na kumpitisha, kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2010 kifungu cha 30 sura ya 343.

Mazingira haya yanasababisha wagombea ambao hawana uhusiano na vyama kukosa nafasi ya kufika bungeni au kuingia Ikulu, hivyo kuwa chanzo cha migogoro kama hiyo.

Ili kufanikisha mchakato wa kidemokrasia unaompa kila raia wa Tanzania haki ya kushiriki masuala ya kisiasa pengine ni wakati wa kuruhusu wagombea binafsi.

Mvutano baina ya CHADEMA na bunge unaonekana kuwa unaweka wazi haja ya kuruhusu wagombea hao.

Ibara za 21, 39, 47 na 67 ya katiba ya Tanzania ndiyo msingi wa haki ya wachache (wabunge au madiwani) kuwawakilisha wananchi katika bunge au udiwani.

Ndiyo ibara inayoweka vigezo kuwa ni lazima uwe mwanachama na kudhaminiwa na chama cha siasa bila hivyo huwezi kuwa mbunge au diwani.

Ibara ya 71(1)(e), inabainisha kuwa mbunge atakoma kuwa mwakilishi wa wananchi wake endapo ataacha kuwa mwanachama wa chama alichopitia kuingia bungeni.

Wabunge hao 19 wa CHADEMA



Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alitangaza msimamo wa kuwafukuza uanachama wabunge 19 wa viti maalum. **PICHA: MTANDAO**

ambao wameapa kuwa wabunge wa viti maalumu na ambao bunge linawatambua wamevuliwa uanachama na CHADEMA.

Kufukuzwa uanachama kunamaanisha uwakilishi wao kwa mujibu wa katiba umekoma kwa kuwa ibara ya 71(1)(e) inawaondolea uhalali wa ubunge. Kwa hiyo chama wakitumia kipengele cha katiba wanakuwa sahihi.

### TUME KUWAPA UHALALI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC, taasisi ya umma yenye majukumu mengi kisheria mojawapo ni kusimamia na kuratibu uendeshwaji wa uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani Tanzania Bara wakati Zanzibar inasimamia uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na wabunge.

Ibara ya 74 (11) ya katiba, inasema katika kutelekeza majukumu yake NEC haitafuata amri au maelekezo ya yeyote, idara ya serikali au maoni ya chama chochote.

Na kwenye ibara ya 74 (12) inasema NEC ikishatekeleza majukumu yake, hakuna mahakama yoyote itakayohoji. Ndiyo uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo imefikisha bungeni majina wabunge hao wa viti maalumu

> “Mkataba huo wa viongozi wa Afrika kwa pamoja wanakubaliana kuusaini na kutekeleza ili kuheshimu haki za binadamu, kufanya uchaguzi ulio huru na haki, kuhakikisha uongozi bora, kutoa nafasi ya watu kushiriki masuala mbalimbali kuanzia siasa, uchumi na uongozi bila kunyimwa haki za msingi kama kujieleza na uhuru wa maoni.

na wameapa hakuna wa kuwatengua wala kuwaondoa kwenye nafasi hiyo.

Licha ya kuonekana kuwa kuna changamoto za kikatiba, uhuru huo wa NEC hauwezi kutetereshwa na msimamo wa CHADEMA wa kuwafutia uanachama wabunge 19 wa viti maalumu hivyo watabaki kama ilivyo.

### WAPI TUME HURU?

Majukumu ya NEC yanayotajwa kwenye katiba kuanzia ibara ya 5 hadi ya 98, mengine yako kwenye Sheria ya Uchaguzi na hata za Uchaguzi ya Serikali za Mitaa hata suala la kufikisha majina bungeni, yana uhalali wa kisheria na tume iko huru, lakini kinacholalamikiwa kila leo ni uteuzi wa uongozi na utendaji kazi wa tume hiyo, ikidaiwa kuwa haina uhuru unaotajwa kikatiba.

Hilo limekuwa ni lalamiko kubwa kutoka vyama vya upinzani na pia asasi za kiraia, wadau wa uchaguzi wa kimataifa na kikanda na kutaka iundwe tume huru ambayo wajumbe wake hawatokani na serikali licha ya kwamba kikatiba tume hiyo, imepewa uhuru kamili.

Lakini, ukiangalia, baadhi ya mataifa ya Afrika kama Kenya, Afrika Kusini na Ghana yanaelezwa kuwa yana tume huru inayoruhusu kuwapo uchaguzi huru na haki hata hivyo, ukweli ni kwamba hakuna tume ya uchaguzi ambayo inafanyakazi bila lawama.

Mathalani Tume ya Ghana ambayo haiteuliwi na serikali ilionekana kuwa ni bora na ya mfano, lakini bado imetwishwa lawama kwenye uchaguzi wa mwezi uliopita uliowashindanisha wagombea Rais wa zamani John Mahama na Rais wa sasa John Akufo Addo, Chama cha Mahama kinalalamikia kuwa ulijaa udanganyifu na wizi wa kura.

Kenya, tume yao iliandaliwa baada ya kuandika katiba mpya na hateui wala kuhusika na mchakato wa watendaji ambao unafanywa kwa uwazi, bado inalalamikiwa.

Kilichoshangaza dunia ni uchaguzi wa karibu mwezi mmoja uliopita huko Marekani rais anayeondoka madarakani Donald Trump, analalamikia hujuma na kulaumu kuwa vyombo vya kusimamia uchaguzi majimboni vimempora ushindi na kumpa Joseph Biden, hili linatazamwaje?

### UKIMYA UISHE

Kinachoonekana hapa ni mkanganyiko kisheria na kikatiba. Cha msingi ni kuandaa katiba mpya tena kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU), ambao kwenye eneo la demokrasia hasa kuwa na tume huru, kutoa haki ya kuwa na wagombea huru na matokeo ya uchaguzi kupingwa ni masuala yanayotajwa kwa nguvu zote.

Yote yamo kwenye Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi (ACDEG). Pengine hayo ndiyo masuala yanayoweza kutumiwa kuangalia mkanganyiko baina ya bunge, tume, wabunge wa viti maalumu wa CHADEMA wanaolumbaniwa.

Mkataba huo wa viongozi wa Afrika kwa pamoja wanakubaliana kuusaini na kuutekeleza ili kuheshimu haki za binadamu, kufanya uchaguzi ulio huru na haki, kuhakikisha uongozi bora, kutoa nafasi ya watu kushiriki masuala mbalimbali kuanzia siasa, uchumi na uongozi bila kunyimwa haki za msingi kama kujieleza na uhuru wa maoni.

Aidha, mkataba huo una vipengele vya ulinzi wa mali ya umma na kuondoa rushwa na kudumisha utawala wa haki na sheria.

Ni vyema kuutizama na kurekebisha katiba ya 1977 kuwezesha kusaini na kutekeleza ACDEG ambayo mambo makuu yaliyoko ndani yake ni kufanyika uchaguzi huru na haki, kuruhusu matokeo ya uchaguzi kupingwa mahakamani, kuwapo kwa wagombea binafsi au huru na kutoa nafasi kwa vyama vya siasa kufanya kampeni zake kwa uhuru na kutoa nafasi sawa na za haki kwa upinzani kutumia jukwaa hilo kujitangaza na kuendesha kampeni.

Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za uchaguzi kuendelea kubaki kama ilivyo kunaweza kuendeleza miongo kadhaa ya figisu zinazoibuka baada ya uchaguzi kila wakati. Ni muda wa kuamua la kufanya kama taifa, kutafakari na kuchukua hatua.

# PROFESA MBILINYI 1938 -2020

## •Ameacha mengi darasani na serikalini



Profesa Simon Mbilinyi akiwa na Balozi wa Tanzania Marekani, Dk. Asha-Rose Migiro, katika moja ya mikutano enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

MAMIA ya wakazi wa jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki walikuwa katika maombolezo ya kumuaga na kumfikisha katika nyumba ya milele, gwiji wa uchumi kitaifa, Profesa Simon Mbilinyi.

Huyo ni mchumi wa siku nyingi, akiwa na mzizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mshauri mwandamizi serikalini, balozi nchi za Ulaya, Mbunge wa Jimbo la Peramiho na kwa muda mfupi Waziri wa Fedha, 1995 hadi 1996, Rais Benjamin Mkapa, alipokuwa anaanza jukumu lake.

Hata hivyo, alijiuzulu ndani ya mwaka mmoja pamoja na Naibu wake Kilontsi Mporogoromyi, wakati upinzani ulijikita katika 'kulipua mabomu' ya kashfa ya kisiasa iliyoangukia mikononi mwao.

Ni aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Augustine Mrema, aliyelipua bomu la 'hongo inayotokana na mauzo ya minofu ya samaki,' Bunge likaona mbadala wa majibu ya haraka ni waziri na naibu wake wajiuzulu.

Baada ya hapo alibaki kisiasa katika Jimbo lake la Peramiho alikochaguliwa ubunge, hadi kufikia mwaka 2010 alipostaafu na kuendelea na kazi nyingine sekta za umma.

Alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Huria kwa miaka saba, 2002 hadi 2009 na mmoja wa washauri waandamizi katika masuala ya uwekezaji wakati wa awamu ya tatu, kutokana na uzoefu wake na taasisi tofauti nchi za Ulaya ambako alipokuwa balozi za Ubelgiji na Luxemburg mwaka 1985 hadi 1989.

Ni wakati Tanzania ilipoingia katika mabadiliko makubwa kutoka uchumi wa kijamaa (uzalishaji kusimamiwa na serikali) kwenda uchumi wa soko, unaoshirikisha kwa upana zaidi jitihada sekta binafsi.

Taarifa zinaonyesha kuwa wakati wa ujana wake alikuwa mshirika wa kampuni ya Xerox (kufyatua nakala) kabla ya utaifishaji wa Azimio la Arusha la mwaka 1967, kikitajwa kipindi kati ya mwaka 1960 hadi 1966.

Alianza fani yake ya uchumi, katika miaka ya 1950 alikuwa katika Chuo Kikuu cha Cornell (Ithaca, New |York) halafu Chuo Kikuu cha Stanford (California), vyote vya Marekani na alikamilisha utafiti na tungo ya uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mwandishi wa makala akiwa kijana wastani wa miaka 40 iliyopita katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alishasoma utafiti wa Profesa Mbilinyi mwaka 1967 unaogusia 'biashara ya machungwa jijini Dar es Salaam,' moja ya utafiti uliojenga mazoea ya ufuatiliaji wa mwingiliano ya kiuchumi kati ya maeneo ya vijijini na mijini.

Baada ya kupitia hatua kadhaa za kitaaluma, mwaka 1977 alishafikia ngazi ya uprofesa, hapo alikwezwa katika jukumu la kiuchumi, kumpokea Profesa Justinian Rweyemamu, katika kazi ya Mshauri wa Uchumi wa Rais Julius Nyerere.

Profesa Rweyemanu, aliyejulikkana hata kifikra kuwa mjamaa kamili, sehemu ya jihuda zake zilizama katika mauzo ya mazao ya kilimo nje, ili kujenga msingi wa viwanda nchini.

Kazi hiyo ya ushauri, inaelezwa kubuniwa na Mwalimu alipoianza na Profesa Knud Erik Svendsen, kutoka Denmark, Tanzania ikishamiri katika Ujamaa kuanzia katikati ya miaka ya 1960 hadi mwanzoni mwa 1970.

Baadaye, msomi huyo wa kigeni alitwisha mambo mengine, ikiwamo jukumu la kuongoza taasisi ya utafiti uchumi ya REPOA aliyokuwa nayo hadi mwaka 2013.

Mwaka 1977 ambao kiuchumi unakumbukwa kuwa ni zama nchi ilipofanya mazungumzo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), ikiwamo katika namna ya kujaza mapengo ya bajeti.

Profesa Mbilinyi alibakia hapo hadi awamu ya pili ya uongozi wa nchi, ndipo Profesa Ibrahim Lipumba alipoteuliwa kuchukua nafasi na baadaye, Dk. Juma Ngasongwa.

Profesa Mbilinyi wakati akiwa anasoma nchini Marekani kusoma shahada ya kwanza na ya pili, alifunga ndoa na raia wa nchi hiyo na wakarudi nchini.

Mama huyo ameongezeka kwa hulka ya ziada, kwamba licha ya kutokea katika jamii ya kigeni, amekuwa mahiri katika kumudu lugha za asili, ikiwamo ya mumewe - Kinyakyusa, akipambana katika stadi ya lugha mithili ya wenyeji, kiasi cha kutengeneza mvuto ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kisingi, alijikita katika fani ya lugha, labda ikawa daraja la kuufikia uzalendo kwa urahisi zaidi, tofauti na mtiririko wa nukuu za vitabu na mada kila mwezi mmoja au mwili ziitwazo za 'Marjorie Mbilinyi'. Ni sehemu ya mwingiliano wa kitamaduni iliyojenga taswira ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na taifa.

Wakati ametutangulia, mchumi huyo anabaki kuwa na mchango unaobeba historia muhimu katika kuchangia maendeleo ya taifa.

***Burian Mbilinyi.***

## YA UNGUJA YANABAMBA

1. Ya Unguja yanabamba,
Hiyo raha hadi Pemba,
Wote sasa ni wajomba,
Kusiwepo kusutana.

2. Tulikuwa tunaomba,
Kutoka kwake Muumba,
Vile alivyotuumba,
Kusiwepo kusutana.

3. Wa mjini hata shamba,
Hata mji kule Fumba,
Tulitaka ile nyumba,
Kusiwepo kusutana.

4. Uchaguzi tuliyumba,
Na kuchafuliwa pamba,
Sote sasa tuko chemba,
Kusiwepo kusutana.

5. Wapo tuliowasomba,
Kwamba mjini watamba,
Sasa hata wale njemba,
Kusiwepo kusutana.

6. Mkuu wimbo kaimba,
Aina ya kwake nyumba,
Ili asiweze yumba,
Kusiwepo kusutana.

7. Mkwara waliuchimba,
Na maneno wakagomba,
Wakatulizana chemba,
Kusiwepo kusutana.

8. Mungu katupa Zanzibar,
Unguja ongeza Pemba,
Nchi moja tunatamba,
Kusiwepo kusutana.

9. Hussein hajawa mwamba,
Peke yake akitamba,
Kaka yake kamuomba,
Kusiwepo kusutana.

10. Maalim kule chemba,
Akailegeza kamba,
Ili Unguja na Pemba,
Kusiwepo kusutana.

11. Muda wa nyimbo kuimba,
Na barabara kuchimba,
Tuicheze hata samba,
Kusiwepo kusutana.

12. Pamoja tujenge nyumba,
Kwa fito kutoka shamba,
Msingi tukiuchimba,
Kusiwepo kusutana.

13. Twawahongera Zanzibar,
Hebu fukiza uvumba,
Acha tusakate rumba,
Kusiwepo kusutana.

14. Mwinyi, Maalim tamba,
Na Hemed jenga nyumba,
Visiwani kuwe bomba,
Kusiwepo kusutana.

15. Chini chini kuna myamba,
Kufika hapa twatamba,
Wamefanya vema kwamba,
Kusiwepo kusutana.

16. Vyama viwili sambamba,
Vimejitoa kimwamba,
Wameziacha kasumba,
Kusiwepo kusutana.

17. Zitto tusipomuimba,
Tutakuwa ni wa shamba,
Kaongoza kule chemba,
Kusiwepo kusutana.

18. Chama kichanga chatamba,
Makamu ndani ya nyumba,
Dume wameshalilamba,
Kusiwepo kusutana.

19. Magufuli naye mwamba,
Na mkali kama simba,
Hili wala hajayumba,
Kusiwepo kusutana.

20. CCM ingetamba,
Pekee kujenga nyumba,
Uamuzi wao bomba,
Kusiwepo kusutana.

21. Viongozi ni miamba,
Wanataka jenga nyumba,
Wa Unguja na Pemba,
Kusiwepo kusutana.

22. Wananchi wa Zanzibar,
Sasa wao ni miamba,
Watoke wacheze samba,
Kusiwepo kusutana.

23. Vidonda vilivyovimba,
Na maneno ya kugomba,
Yote tujifunge pamba,
Kusiwepo kusutana.

24. Tuombe kwake Muumba,
Kusitokee kizimba,
Tuweze kujenga nyumba,
Kusiwepo kusutana.

25. Sitini na nne imba,
Mapinduzi yalitamba,
Waafrika kwenye dimba,
Kusiwepo kusutana.

26. Tukukatae kuyumba,
Tunajenga moja nyumba,
Tuzikate kamba kamba,
Kusiwepo kusutana.

27. Tarehe nane Disemba,
Jumanne tunatamba,
Kata kata tunaimba,
Kusiwepo kusutana.

***Lwaga Mwambande (KimpaB)***

# PROFESA MOHSEN FAKHRIZADEH:

## •Gwiji wa nyuklia aliyeuawa kwa bomu
## •Tegemeo la Iran kufikia chanjo corona

Na Ani Jozeni

KIZA kimetanda katika nchi kadhaa baada ya kuuawa kwa mbinu za kijasusi za Profesa Mohsen Fakhrizadeh, anayetambuliwa kama mtafiti mkuu na mwendeshaji wa mpango wa nyuklia wa Iran.

Kwanza kwa ajili ya kuendesha mitambo ya umeme halafu pia kuunda zana za nyuklia.

Aliuawa Novemba 27 nje ya jiji la Tehran licha ya kuwa na msafara ambao ni pamoja na magari ya deraya yasiyopenya risasi kwa mujibu wa walioelezea tukio hilo.

Walidai kuwa alionywa asisafiri nje ya Tehran na kifo chake ni pigo kubwa kwa uendelezaji wa mpango huo wa nyuklia na hata wa chanjo, licha ya kutofahamiki hazina Iran ya wanasayansi wa ngazi hiyo, kwani Israel imekuwa ikiwawinda ili kuwaua.

Si Marekani wala Israel ambayo ilitangaza kuhusika na kifo hicho, ila baadhi ya walioelezea tukio hilo kwenye mitandao wanaamini mahasimu walitumia au angalau kuwahusisha Mujahedeen el-Haq, kundi la kimapinduzi hasimu.

**HISTORIA TAALUMA**

Fakhrizadeh alizaliwa 1958 katika mji wa Qom ambako pia wanatokea viongozi wakuu wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, akiwamo Hayati Ayatollah Ruhollah Khomeini na mrithi wake, Ayatollah Ali Khamenei.

Amekuwa sehemu ya kundi la ulinzi wa mapinduzi ya Iran ambalo hasa ndiyo jeshi la nchi hiyo baada ya jeshi la jadi kusambaratishwa, na hata kufikia ngazi ya brigedia-jenerali.

Waandishi wa habari hizo katika kituo cha Begin-Sadat cha utafiti wa mikakati ya kijeshi Mashariki ya Kati, waliorodhesha safari alizofanya Fakhrizadeh hasa nchini Korea Kaskazini, ambako mara kadhaa alikuwapo wakati wa kulipua mabomu ya majaribio ya silaha za nyuklia.

Baadhi wanasema kuwa Korea Kaskazini ilipata 'siri' za kuunda bomu la nyuklia kutoka Pakistan na kuwa Iran imekuwa ikiitegemea zaidi Korea Kaskazini, labda kwa michoro na miundombinu mingine, kwani Fakhrizadeh na wenzie wanaelekea walidhibiti mitiririko ya hesabu kuhusiana na mwelekeo huo.

Profesa Fakhrizadeh alisoma nchini Iran na hakuna vielelezo kuwa kuna wakati alikuwa nje, kwani wakati alipokuwa anaingia chuo kikuu ndiyo wakati mapinduzi yalikuwa yanapamba moto, mwaka 1979 akiwa na umri wa miaka 21. Alisomea Chuo Kikuu cha Shahid Beheshti na kupata shahada ya uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Isfahan mwaka 1991, akawa profesa wa fizikia Chuo Kikuu cha Imam Hossein. Aliongoza shirika la ubunifu na utafiti sekta ya ulinzi na mradi wa utafiti nuklia.



**CHANJO YA CORONA**

Aliwekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa na Marekani katika miaka ya 2005 na kwamba licha ya kufahamika kwa mashirika ya kijasusi kuendesha mpango wa AMAD unaohusu kuinua uwezo wa silaha za nyuklia, aliongoza utafiti chanjo ya corona.

Eneo muhimu zaidi linaloangaliwa kufuatia kuuawa kwa mtaalamu huyo asiye na mwenza nchini Iran, ni uwezo wa nchi hiyo kufuatilia mipango yake ya nyuklia bila ya uongozi na uratibu aliokuwa akiusimamia.

Yako maeneo mengine ambayo watafiti wa masuala ya kijasusi wanayaangalia kwa karibu. Kituo cha Begin-Sadat nchini Israel kwa mfano kilifuatilia kwa makini upokeaji na mwitikio wa wananchi wa Iran kwa mauaji hayo, na hasa kuangalia idadi ya wananchi waliojitokeza katika maandamano yaliyoandaliwa na dola ya kimapinduzi kushutumu mahasimu wao kwa mauaji hayo. Wanasema idadi haikuwa kubwa.

Wanaunganisha uhaba huo wa kuwalilia walio karibu na utawala wa serikali wanapofikwa na 'ajali za kijasusi' kama aliyekuwa mkuu wa operesheni za nje za majeshi ya Iran, Jenerali Qassem Soleimani, aliyeuawa kwa kombora lililoshushwa na ndege isiyo na rubani ya Marekani mwaka jana.

Inadaiwa kuwa watu wenye silaha waliushambulia msafara wake na watatu wakauawa, baada ya gari lililotegwa njiani kulipuliwa, ili kuzuia msafara huo.

Taarifa nyingine zinasema kuwa kulikuwa na gari lenye bunduki likiongozwa kutoka mbali lililipuliwa baada ya tukio hilo.

> Kuna eneo lingine ambalo halijazungumziwa sana na hasa kutokana na mabadiliko ya utawala nchini Marekani na wengi kati ya walio karibu na rais mteule Joe Biden kutaka kurudi katika mkataba wa kuzuia Iran kuendelea na utafiti wa silaha za nyuklia.

Kuna eneo lingine ambalo halijazungumziwa sana na hasa kutokana na mabadiliko ya utawala nchini Marekani na wengi kati ya walio karibu na rais mteule Joe Biden kutaka kurudi katika mkataba wa kuzuia Iran kuendelea na utafiti wa silaha za nyuklia.

Rais Donald Trump, aliiondoa Marekani katika mkataba huo mwaka 2018 na kuuawa kwa Fakhrizadeh na hasira za Iran kunaleta changamoto mpya kwa utawala unaoingia madarakani kuanzia Januari 20.Bunge la Marekani limegawanyika kuhusu jambo hilo.

Eneo jingine ni mawasiliano ya karibu kati ya Israel na Saudi Arabia kabla ya tukio hilo, ambako Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu alifika Jeddah ili kuzungumza na mwanamfalme Mohammed bin Salman.

Uhusiano unaimarika kati ya Falme za Mashariki ya Kati na Israel, lakini wanaharakati nchini Marekani bado hawaridhiki wakiwa na mbadala wao.



# Walimu wa dini shuleni wafundwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WALIMU wanaofundisha masomo ya dini katika shule za msingi na sekondari za serikali, wametakiwa kuwaelekeza na kuwajengea maadili mema watoto hao ili kuwa mfano mwema katika jamii.

Katibu wa Taasisi ya Dodoma General Muslim Assoaciation (DGMA), Twalib Twalib, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja ya walimu wanaofundisha vipindi vya elimu ya dini ya kiislamu shuleni Mkoa wa Dodoma.

Twalibu aliwataka walimu hao wanaofundisha watoto waliopo kwenye shule za serikali kuhakikisha wanawajengea na kuwafundisha maadili mema ili kuwa raia wema.

"Ndugu zangu siku hizi kumekuwa na malalamiko kwenye jamii kuwa watoto wetu wameharibika, mjue kuwa kazi ya kuwatengeneza mnayo ninyi walimu, hakikisheni mnawafundisha maadili mema," alisema.

Alisema walimu wa dini wanaofundisha shuleni wana nafasi kubwa ya kusaidia kuwajengea watoto maadili mema kwa sababu ya kuwafundisha neno la Mungu.

"Mtoto aliyelelewa vizuri kwenye neno la Mungu ana hofu ya kufanya maasi katika jamaii kwa kujua kuwa Mungu anamuona kila mahali," alisema.

Kadhalika, alisema walimu hao wanao wajibu wa kuhakikisha wanafundisha kila kipindi kama walivyopangiwa na shule husika na wasikose kwa sababu serikali inaheshimu dini ndio maana wakapanga vipindi hivyo.

Aidha, alisema kutokana na tatizo la uhaba wa walimu wa dini hiyo, kwenye shule hizo, taasisi hiyo imeona ichukue jukumu la kuwajengea uwezo walimu hao ili kusaidia vipindi hivyo.

Alibainisha kuwa walimu hao waliopatiwa mafunzo hayo watawajibika kutoa huduma hiyo kwenye shule za serikali, ili kuhakikisha watoto wanajifunza kwenye vipindi hivyo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Ismail Dawood, alisema lengo lao ni kuhakikisha wanatoa mafunzo kwa walimu wengi ili kuzifikia shule nyingi zaidi.

"Mkoa una shule nyingi za serikali za msingi na sekondari, jukumu hilo la kuwafundisha watoto elimu ya dini wakiwa shuleni linahitaji watu wa kujitolea kwa sababu malipo yake ni makubwa huko Akhera," alisema.

Dawood alisema taasisi hiyo pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu hao pia inawapatia vitabu vya kufundisha elimu hiyo ya dini kwa shule za msingi na sekondari.

Pia, aliwataka walimu hao kuwa mfano mwema wa maadili kwa watoto hao wanaowafundisha ili kuingia mwenendo huo.

# Hakielimu yabainisha kasoro shule watoto wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

**Ili shule za elimu jumuishi ziweze kuondokana na kero, serikali na wadau wa elimu ni muhimu wakatenga bajeti ya kutosha ambayo itasaidia kuondoa kero hizo zilizopo kwenye shule.**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Hakielimu, Dk. John Kelegeni, amesema miundombinu na mitaala kwenye shule zinazojumuisha watoto wenye mahitaji maalumu bado haikidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

Pia, uwezo wa walimu wenye sifa na taaluma ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu kwenye shule za elimu jumuishi bado zinahitajika kufanyiwa maboresho.

Dk. Kalegeni alisema hayo kwenye kongamano lililowakutanisha wadau wa elimu jumuishi lililoandaliwa na mradi wa elimu wa Kanisa la Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT) jijini Dodoma.

Alisema kuwa miundombinu hiyo bado inahitajika kufanyiwa maboresho makubwa ili watoto wenye ulemavu wafikie malengo yao katika kufanya vizuri kimasomo.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa jamii bado kuna familia zenye watoto wenye ulemavu, ambao hawana uelewa wa kufikiri umuhimu wa kuwapeleka kuwaandikisha shule kwa mitizamo hasi kuwa hawawezi kupata faida yoyote hata kama watasoma.

Alisema ili kuondoa kero hizo, wadau na serikali ni muhimu wakaelekeza nguvu zao kwa ajili ya kuhakikisha kero zilizopo kwenye shule hizo zinatatuliwa na hatimaye wanapata haki zao za msingi za elimu.

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Ansila Mavandu, aliiomba serikali na wadau wa elimu kuwekeza kwa nguvu zote kwenye mpango mkakati wa elimu jumuishi, ili watoto wenye ulemavu wapate elimu itakayowawezesha kufikia malengo.

Mavandu alisema ili shule za elimu jumuishi ziweze kuondokana na kero, serikali na wadau wa elimu ni muhimu wakatenga bajeti ya kutosha ambayo itasaidia kuondoa kero hizo zilizopo kwenye shule.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT), Askofu George Mwita, alisema kwa upande wao wataendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuendeleza sekta ya elimu, ili kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi katika Jiji la Dodoma.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu, kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu kielimu ili nao waweze kupata haki yao ya msingi ya elimu kama watoto wengine.



Ofisa Elimu Maalumu wa Jiji la Dodoma, Agnes Mwingira, akizungumza na wadau wa Elimu Jumuishi kwenye kongamano lililoandaliwa na mradi wa elimu jumuishi toka kanisa la FPCT Wilaya ya Dodoma na Bahi kwa ajili ya umuhimu wa kuchangia uwekezaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu kupata haki zao za kimsingi za elimu lililofanyika Dodoma jana (juzi). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kikwazo mapambano dhidi ukatili wa kijinsia chatajwa

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

USHIRIKIANO mdogo kati ya wazazi na walimu umetajwa ni moja ya sababu inayokwamisha juhudi za mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, mimba na ndoa za utotoni katika Wilaya ya Chamwino.

Hayo yalibainishwa juzi na mwalimu mlezi wa klabu ya kupinga ukatili wa kijinsia, mimba na ndoa za utotoni, Gift Rupia, katika kikao cha tathmini ya kubaini changamoto zinazokabili mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia katika mradi wa kutokomeza mimba za utotoni unatekelezwa na Shirika la Women Wakeup (WOWAP) wilayani humo.

Mwalimu Rupia alisema kumekuwa na ushirikiano mdogo kati ya pande hizo mbili kutokana na baadhi ya wazazi kutozungumza na watoto wao juu ya afya ya uzazi.

"Ushirikiano bado ni changamoto kati yetu sisi na wazazi kwa sababu unakuta binti anapata ujauzito, unamtafuta mzazi uongee naye, ili mjue unamsaidiaje binti, lakini cha ajabu mzazi anarusha mpira kwa mwalimu kuwa hakuwajibika," alisema Rupia.

Alisema, baadhi ya wazazi hawako wazi kwa watoto wao, kutokana na kuwa bado wana mila na desturi zinazowafanya washindwe kuongea na watoto wao kuwaambia juu ya madhara ya kupata mimba katika umri mdogo.

Kutokana na hili alisema waelimishaji rika wanapaswa kupita kaya kwa kaya ili kutoa ushauri kwa wazazi waongee na mabinti zao na kuwaweka wazi juu ya umuhimu wa afya za uzazi na kuepukana na mimba za utotoni.

"Masuala ya kusema kuwaweka watoto wazi ni mambo ya aibu sasa yamepitwa na wakati, usipomfundisha," alisema.

Mratibu wa Wowap, Nasra Suleiman, alisema kwa sasa wanaendelea na uelimishaji kuhusu uwajibikaji kwa viongozi wa maeneo husika, ili wanapokutana na matukio ya aina hiyo yashughulikiwe, jambo ambalo litaongeza imani kwa wananchi na kutoa taarifa zaidi.



# Wananchi wapewa mchongo fursa uwekezaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPUNI ya Uwekezaji wa Pamoja (UTT AMIS), imewataka wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia fursa za kuwekeza kwenye mifuko ya pamoja kwa kuwa ina mfumo mzuri wa usimamizi wa fedha ambao unawahakikishia usalama wa mali zao.

Mkuu wa Masoko wa UTT AMIS, Daud Mbaga, aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuhudumia wawekezaji. Alisema mali za mifuko hiyo ziko chini ya uangalizi wa Benki ya CRDB na kwamba ziko salama.

Aliwataka wananchi wanaotamani kuwekeza kuondoa fikra kwamba wanaweza kupoteza mali zao kama ilivyowahi kutokea kwa waliokuwa wamewekeza kwenye kampuni kama DECI miaka ya nyuma ambako wengi walipoteza fedha zao.

**Mpaka Desemba, mwaka huu, mali kwenye mifuko zina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 478 na kwamba zinaendelea kuongezeka kutokana na wawekezaji kuongeza uwekezaji wa mali.**

Mbaga alisema UTT AMIS ni mali ya ya serikali na iko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Alisema mpaka sasa inasimamia mifuko sita ya uwekezaji ambayo ni Mfuko wa Umoja, Wekeza Maisha, Watoto, Jikimu, Ukwasi na Hati Fungani.

"UTT AMIS inatekeleza majukumu yake kulingana na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 na marekebisho yake pamoja na kanuni za mifuko ya uwekezaji wa pamoja za mwaka 1997, hivyo ni kampuni ambayo inatambuliwa na sheria, wananchi wasiogope kuwekeza," alisema Mbaga.

Alisema kampuni hiyo iliamua kufungua kituo jijini Mbeya kutokana na maombi ya watu wengi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambao walikuwa wanaomba wasogezewe huduma hiyo.

Mkuu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Takwimu wa UTT AMIS, Sophia Mgaya, alisema moja ya vigezo vya kupima utendaji na ufanisi wa kampuni ni wingi wa rasilimali ambao umekifikia na kwamba ndiyo maana inaaminiwa.

Alisema mpaka Desemba, mwaka huu, mali kwenye mifuko zina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 478 na kwamba zinaendelea kuongezeka kutokana na wawekezaji kuongeza uwekezaji wa mali.

Pia alisema kumekuwapo na ongezeko la matumizi ya fedha kupitia njia ya mitandao na kwamba fedha zinazopitia kwenye mitandao zimefikia Sh. milioni 300 kwa mwezi na kwamba wanaendelea kuta elimu ya matumizi ya simu.

Aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuweka mazingira na misingi mizuri ya dhana ya uwekezaji wa pamoja ambayo imekuwa kivutio cha watu wengi kujiunga na mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

"Tunaishukuru pia Benki ya CRDB kwa kutunza mali za wawekezaji na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa kuhakikisha kanuni zote za husika katika uwekezaji wa pamoja zinafuatwa bila kusahau madalali na wadau wote wa masoko ya hisa na mitaji," alisema Mgaya.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini (TCRA-CCC), Mary Msuya (kulia), akitoa elimu ya matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano kwa watumiaji pamoja na fursa zinazopatikana kwenye huduma hizo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Walia ubovu wa barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Kikondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kuiboresha barabara ya Isyonje- Kikondo ili kuwapunguzia gharama za usafiri na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali yakiwamo mazao ya kilimo.

Walitoa ombi hilo juzi, walipokuwa wanazungumza na Nipashe kuhusu matatizo mbalimbali yanayowakabili, ambapo walisema tatizo la barabara ndilo linalowatesa kwa muda mrefu hasa kipindi hiki cha mvua ambapo baadhi ya maeneo huwa hayapitiki.

Mmoja wa wananchi hao, Jota Ng'anya, alisema kijiji hicho ni miongoni mwa vijiji vinavyoongoza kwenye uzalishaji wa viazi mviringo, lakini wanashindwa kupata faida nzuri kwenye kilimo hicho kutokana na ubovu wa barabara.

Alisema kutokana na tatizo hilo huwa wanalazimika kusafirisha viazi hivyo kwa kutumia pikipiki mpaka karibu na Isyonje ndipo wanunuzi wapakie kwenye magari na kusafirisha kwenda maeneo mbalimbali ya masoko.

Naye Maria Mwasapile, alisema wakati mwingine huwa wanapata shida ya kuwasafirisha wagonjwa kutoka kijijini hapo kwenda katika hospitali zilizoko Mbeya Mjini kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa sababu mbali na kuwasaidia wao, lakini pia inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Alisema wagonjwa wengi wanasafiri kupitia barabara hiyo, kwenda katika Hospitali ya Misheni ya Ikonda iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete mkoani Njombe.

# Wataka Tukuyu kuwa halmashauri ya mji

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, limeomba serikali kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji wa Tukuyu kuwa Halmashauri ya Mji ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Mbunge wa Rungwe, Anthon Mwantona, aliwasilisha ombi hilo wakati wa kikao cha kwanza cha baraza hilo, ambacho kilikuwa kimeandaliwa kwa ajili ya kuwaapisha madiwani. Alisema jimbo hilo linastahili kuwa na halmashauri mbili kutokana na ukubwa wake.

Alisema kuupandisha hadhi mji huo kutasaidia kuongeza huduma kwa wananchi kwa maelezo kuwa hata huduma za afya zitasogea zaidi kwa wananchi kutokana na utaratibu wa serikali kujenga Hospitali ya Wilaya katika kila halmashauri.

Mwantona alisema hata ujenzi wa ofisi mpya za Halmashauri ya Mji wa Tukuyu utasaidia kuwapunguzia wananchi tatizo la kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za serikali katika Ofisi za Halmashauri ya Rungwe.

"Nimeambiwa kwamba mchakato wa kupandishwa hadhi kwa mji wetu huu umefika katika ngazi mbalimbali, hivyo itakuwa kazi yangu kufuatilia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ili kufanikisha jambo hili," alisema Mwantona.

Alisema wakati wa kampeni alibaini kuwa mji huo unastahili kupandishwa hadhi kutokana na mahitaji ya wananchi kuwa makubwa na kwamba alipoanza kufuatilia alibaini kuwa mchakato ulishaanza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter, alisema mchakato wa kuipandisha ulianzia kwenye vikao vya Baraza la Madiwani wa Halmashauri, Kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC) na Kikao cha Ushauri cha Mkoa (RCC).

Alisema mji huo kwa sasa tayari una vigezo vya kupanda hadhi na hivyo ana uhakika kuwa wizara itakubali kuupandisha hadhi kutokana na serikali kuwa na uhitaji wa kusogeza huduma kwa wananchi kulingana ukubwa wa maeneo yao.

"Tutashukuru sana endapo serikali itakubali kupandisha mji huu. Hii itatusaidia kusogeza huduma kwa wananchi. Sisi tumetekeleza wajibu wetu kadri tulivyoweza, RCC pia walifanya wajibu wao na walishawasilisha kwenye ngazi za juu," alisema Peter.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanafanya kazi ya kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aliwataka kuwatembelea wananchi mara kwa mara kwenye maeneo yao, ili kujua kero zinazowakabili na kuziwasilisha kwenye vikao vya halmashauri ili zitatuliwe haraka.

## TAMWA yapinga mtuhumiwa ubakaji mtoto wa kumzaa kuachiwa huru

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania, upande wa Zanzibar (TAMWA), kimesema hakijaridhishwa na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wete, Mkoa wa Kaskazinia Pemba kwa kumwachia huru mtuhumiwa aliyembaka mtoto wake wa kumzaa.

Hivi karibuni TAMWA ilipokea taarifa kwamba mtuhumiwa Salim Khamis Ali, maarufu "Panga la Shaba" (43), mkaazi wa Taifu Shehia ya Kinyasini, Pemba aliyembaka mtoto wake wa kumzaa huko Pemba kuachiwa huru kwa madai kuwa taarifa za daktari zimeonyesha kwamba mtoto huyo ni mzoefu katika kufanya ngono tangu awali.

Tukio hilo liliripotiwa katika kituo cha polisi Wete Desemba 6, 2019 na kufunguliwa kesi.

Katika mashtaka ilidaiwa kuwa Salim Khamis Ali alimbaka mtoto wake wa kike aliye chini ya umri wa miaka 13.

Kwa mujibu wa Hakimu wa Mahakama ya Wete Mkoa Kaskazini Pemba, Abdalla Yahya Shamhuni, ni kwamba mtuhumwa alitenda kosa Novemba 30, 2019 saa 3:00 usiku katika eneo la Taifu, na bila ya halali mtuhumiwa huyo alimwingilia mtoto huyo huku akijua kuwa ni mtoto wake wa kumzaa, jambo ambalo ni kosa kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 143 (1) (4) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

Hakimu alisema baada ya kukamilika kwa upelelezi wa kesi hiyo, mahakama imemwachia huru mtuhumiwa Desemba 7, 2020 kwa kile kilichodaiwa ushahidi wa daktari ulionyesha kuwa mwathirika aliwahi kuingiliwa hapo awali.

"Katika maelezo yake daktari alieleza kuwa mwathirika ni mzoefu. Hivyo basi baada ya kupitia vyema ushahidi uliowasilishwa na upande wa mashtaka mahakama imeona kwamba mtuhumiwa si mkosaji wa kosa hilo na inamwachia huru chini ya kifungu cha 220 cha sheria namba 7 ya mwaka 2018, Sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar," alisema Shamhun, Hakimu wa Mahakama ya Wete Mkoa Kaskazini Pemba wakati wa hukumu.

# Rais Mwinyi atengua uteuzi Katibu wa Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametengua uteuzi wa Katibu wa Rais Suleiman Ahmed Saleh, ambaye ameshika nafasi hiyo kwa muda wa siku 40 tangu alipoteuliwa Novemba 4, mwaka huu.

Dk. Mwinyi amefanya uamuzi huo kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu namba 53 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kifungu 12(3) cha Sheria ya Utumishi wa umma namba mbili ya mwaka 2011.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ikulu iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Abdulhamid Yahya Mzee, kiongozi huyo aliyetenguliwa atapangiwa kazi nyingine.

Wakati akiwaapisha mawaziri 13 aliowateua baada ya kuunda Baraza la Mawaziri, Dk. Mwinyi, alisema viongozi aliowateua ambao hawataendana na kasi yake ya utendaji kazi atawaondoa, ili kuchagua wengine watakaoendana na kasi yake.

Kabla ya taarifa hiyo ya utenguzi, Rais Dk. Mwinyi alikutana na ujumbe wa Bodi ya Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC) Ikulu na kusema kuwa serikali anayoiongoza itashirikiana vyema na sekta binafsi kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaimarika zaidi.

**Azma yake ni kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara.**

Alisema azma yake ni kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara.

Aliwataka kutoa ushauri juu ya mamlaka za udhibiti, ambazo zipo nyingi na kuleta mkanganyiko katika ulipaji wa kodi na kuzisisitiza mamlaka hizo kuwa pamoja na eneo moja, ili kuondoa usumbufu.

Alisema azma yake kwa mamlaka ya vitega uchumi Zanzibar (ZIPA) katika kuhakikisha inajumuisha masuala yote muhimu kwa wawekezaji na wahusika wote ni lazima wawepo pamoja ili kurahisisha shughuli zao ikiwa ni pamoja na utoaji wa vibali kwa wawekezaji.

Alieleza haja ya kuwapo kwa mawasiliano kati ya sekta binafsi na serikali kwa kujadiliana pamoja kuzitafutia ufumbuzi changamoto zilizopo na kuitaka bodi hiyo kutafuta uwezo wa kuondoa matatizo katika sekta ya biashara kwa kupanga mambo vizuri.

Kwa upande wa uimarishaji wa viwanda vya ndani, Rais Dk. Mwinyi alieleza haja ya kuvilinda viwanda vya ndani ikiwa ni pamoja na kulipa kodi, ili kupatikana uwezo wa kuviendeleza na hatimaye kuwasaidia wananchi wa Zanzibar hasa katika sekta ya ajira.

Kwa upande wao wajumbe hao walieleza azma yao ya kushirikiana na serikali katika kuimarisha sekta ya biashara Zanzibar.

Kaimu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC), Ali Amour, alieleza jinsi wafanyabiashara walivyofarijika na utayari wa serikali anayoiongoza Rais Dk. Hussein Mwinyi katika kushirikiana pamoja kuuinua uchumi wa Zanzibar.

Alisema kuwa Dk. Mwinyi ameonyesha azma ya ushirikiano kati ya sekta binafsi na ya umma, huku akieleza kwamba wataitumia hotuba hiyo katika vikao vyao kama dira ya kuwapeleka kwenye lengo lililokusudiwa.



Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto ambaye ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar (wa pili kushoto), Simai Mohammed Said, akizungumza na watendaji wa wakala wa chakula, dawa na vipodozi Zanzibar (ZFDA), alipofanya ziara katika ofisi hiyo, Mosamba Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wataka sheria zitende haki kwa watu wote

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI pamoja na taasisi zinazosimamia masuala ya sheria Zanzibar zinapaswa kuangalia kwa kina baadhi ya sheria zinazotumika, ili zinapochukuliwa hatua dhidi ya mtu anayefanya makosa katika uamuzi unaotolewa uwe wa haki bila kusumbua upande mwingine.

Viongozi wa Jumuiya ya Walimu wa Madrasa wanaopinga vitendo vya udhalilishaji Zanzibar, walieleza hayo jana walipofanya mazungumza na Makamu wa Pili wa Rais ofisini kwake Vuga, mjini Zanzibar.

Mjumbe wa Jumuiya hiyo, Nyazige Saidi, alisema yapo matukio ya vitendo vya udhalilishaji katika jamii yanayowahusisha zaidi vijana na inapotokea kuchukuliwa hatua za kisheria dhidi yao anayehusishwa na tuhuma hizo anakuwa mmoja mwingine akiendelea kubakia mitaani.

Nyazige alisema matukio hayo yanapofanyika na kuripotiwa vituo vya polisi kinachoendelea mitaani ni kuibuka kwa chuki, uhasama na hata baadhi ya watu kufanyiana ushirikina kwa familia zinazohusika na matukio hayo.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Omar Said Rajab, alisema jumuiya yao yenye wanachama 50 Unguja na Pemba, imekuwa ikiendeleza harakati za kupinga vitendo vya udhalilishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Rajab alisema wanachama wa jumuiya hiyo wananguvu katika harakati zao kwa kupata ushirikiano kwa baadhi ya wazazi licha ya mazingira magumu wanayopambana nayo kwa baadhi ya matukio wanayoyafuatilia.

Alisema kesi za udhalilishaji zinazotokea mitaani zikiripotiwa katika vituo vya polisi kwenye maeneo ya matukio, huchukua zaidi ya miaka mitatu kutokana na baadhi ya watendaji kukosa uaminifu na kuendeleza ubabaishaji.

Kwa upande wake Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema endapo ushiriki wa jamii utakuwa mzuri kutoa ushahidi kwa kesi hizo, adhabu kali itatolewa kwa watuhumiwa hao.

Alisema janga la udhalilishaji hivi sasa limekithiri na kuleta sura mbaya inayolitia sifa mbaya taifa, jambo ambalo serikali kuu italazimika kumchukulia hatua zinazostahiki mtu yeyote atakayebainika na kutuhumiwa kufanya vitendo hivyo bila ya kujali sifa au umaarufu wa mtu huyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:

**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**TAUDESIA JOSEPH KWEKA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1999-0010/2014** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary TUMO mwaka 2014,eyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**CONTROL NO.9910819937805**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 193/2020**
**Ombi la FARAJA MISANGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu THEOPHIL M. NICHOLAUS**
**KWA YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **05/01/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 15/12/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LAWRENCE ALFRED MATWALANE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 561 AEB** AINA YA MITSUBISH FUSO .
KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI: KA H/RB//430/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**GRACE CPRIAN KIJAZI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 393 CHE** AINA YA **WANHOO.** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI: KAH/RB//436/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RUNJI CONSULTING GROUP LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI **LANDCRUISER PRADO** YENYE NAMBA YA USAJILI **TCD 292 EAC**
**CHASSES NO KDJ1200058279**
ENGINE NO 1KD1179456
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE

**TAARIFA KITUO CHA POLISI ARU/ARU/RB/319146/2020**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Museveni azungumzia kuachia ngazi

**Kampala,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni ambaye anawania muhula wa sita madarakani, amesema kwamba hajaona mtu mwenye uwezo wa kuongoza Uganda kwa sasa.

Amesema ataendelea kuwa madarakani kwa sababu wapigakura nchini humo, bado wanamhitaji kuendelea kuongoza taifa hilo.

Akihutubia viongozi wa chama chake cha National Resistance Movement (NRM) katika Wilaya ya Lukungiri, ambayo ni ngome ya kisiasa ya aliyekuwa mpinzani wake mkuu mara nne, Dk. Kiiza Besigye, alisema wapinzani wake ni wazembe wanaotaka kusukumwa kama mkokoteni.

Kati ya wapinzani wake 10 katika uchaguzi mkuu wa mwaka ujao 2021, wapo waliokuwa makamanda muhimu walipokuwa msituni katika vita vilivyomwezesha kuingia madarakani mwaka 1985.

**Nitaondoka tu iwapo kuna mtu wa maana nitakayeona naweza kumwachia Uganda. Nataka niwe na uhakika mahali naiacha Uganda.**

Wagombea hao ni Luteni Jenerali Henry Tumukunde na aliyekuwa Kamanda Mkuu wa Jeshi Meja Jenerali, Mugisha Muntu.

Dk. Besigye si mgombea wa urais katika uchaguzi mkuu mwaka ujao, ingawa anamfanyia kampeni mgombea wa chama chake cha Forum for Democratic Change, Patrick Amuriat.

Dk. Besigye, Tumukunde na Muntu, wanaendelea kufanya kampeni katika sehemu kadhaa za Uganda, wakimtaka Museveni kuondoka madarakani.



Wanadai kuwa Museveni ameshindwa kutekeleza sababu kuu zilizowafanya kuingia msituni na kuanzisha vita vilivyomwezesha kuingia madarakani.

Museveni alisema wanaomkosoa walishindwa na kazi, licha ya kujaribu kila mara kuwaweka katika sehemu tofauti serikalini na sasa wanampigia kelele.

"Wanajua lengo langu katika siasa, lakini wanataka kunishawishi niache msimamo wangu. Wanapiga kelele kwamba nastahili kuondoka madarakani utadhani sina pa kwenda," alisema Museveni akitumia mojawapo ya lugha zinazozungumzwa magharibi mwa Uganda.

Akiwataja watatu hao ambao walikuwa marafiki wake wa muda mrefu na mmoja alikuwa daktari wake binafsi (Dk. Kiiza Besigye), kuwa watu wasiokuwa na maana yoyote.

"Nitaondoka tu iwapo kuna mtu wa maana nitakayeona naweza kumwachia Uganda. Nataka niwe na uhakika mahali naiacha Uganda."

Hata hivyo, Museveni alionekana kumsifu aliyekuwa Waziri Mkuu, Amama Mbabazi na mke wake Jackline Mbabazi akisema kwamba wanafanya vya kutosha kuimarisha kilimo cha majani ya chai.

Museveni alimfuta kazi Amama Mbabazi kutoka nafasi ya waziri mkuu, baada ya kugundua kwamba alikuwa na nia ya kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2016.

Mbabazi aligombea urais na kumaliza katika nafasi ya tatu nyuma ya Museveni na Dk. Besigye akiwa na asilimia moja ya kura. **VOA**

## Boko Haram yadai kuteka wanafunzi

**Katsina,** NIGERIA

KUNDI la kigaidi la Boko Haram, limesema lilihusika na utekaji nyara mamia ya wavulana wa shule katika jimbo la kaskazini magharibi la Katsina State.

Limeeleza, kutekeleza mashambulio hatari katika wiki za hivi karibuni, tovuti ya kibinafsi ya Daily Nigerian, imeripoti.

Mamia ya wavulana wa shule ya sekondari ya serikali, Kankara katika jimbo la Katsina hawajulikani kufuatia shambulio hilo la Ijumaa usiku wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa Daily Nigerian, kiongozi wa Boko Haram, Abubakar Shekau (pichani chini), alisema hayo katika ujumbe wa dakika nne uliyorekodiwa na kundi lililotekeleza shambulio hilo.

"Kwa sababu elimu ya magharibu inaenda kinyume na mafundisho ya Kiislamu. "Kilichofanyika Katsina hi hatua ya kunadi uislamu na kupinga elimu inayoenda kinyume na mafundisho ya dini hiyo, kwani elimu ya magharibi hairuhusiwi na Allah na Mtume wake mtakatifu," tovuti hiyo ilimnukuu Shekau.

Tovuti hiyo ilisema, Shekau hakutoa maelezo kuhusu shambulio hilo, idadi ya wanafunzi waliotekwa au kuthibitisha ripoti kuhusu majadiliano na serikali. **BBC**





Gari iliyokuwa imembeba Naibu Gavana, Mahboobullah Mohebi wa Mji Mkuu wa Afghanstan, Kabul, pamoja na sekretari wake likiwa limelipuka jana na kusababisha vifo vyao, vyanzo vya usalama vimeripoti nchini humo. **PICHA: REUTERS**

## Joe Biden athibitishwa urais Marekani

**Washington,** MAREKANI

JOPO la wajumbe maalumu lenye nguvu ya kumchagua Rais wa Marekani, maarufu Electoral College limemthibitisha Joe Biden, kuwa rais ajae.

Hatua hiyo inatajwa kufunga milango kwa mpinzani wake Donald Trump, katika jitihada zake kisheria kuyageuza matokeo ya uchaguzi wa mwaka huu.

Hatua hiyo inafanyika huku mteule huyo akimkosoa mpinzani wake kwa maneno makali tangu kumalizika kwa uchaguzi kwa kumwita mpinga matakwa ya umma na mkaidi wa katiba ya nchi.

Wakati Biden akipiga kampeni ya kuunganisha taifa, baada ya uchaguzi uliowagawa Wamerekani, wajumbe kutoka majimbo yote.

Biden alifikia hatua ya ushindi baada ya nyongeza ya kura 55 za Jimbo la California pia baada ya Hawaii, kumfanya kuongeza idadi ya kufikia jumla ya kura 306.

Rais wa sasa wa Marekani, Donald Trump alipata kura 232.

Utaratibu wa kura za wajumbe, ambao umedumu kwa takribani miaka 200, umepiga msumari wa mwisho kwa kusema matakwa ya umma yamezingatiwa pamoja na kutokea purukushani za hapa na pale.

Akizungumza baada ya tangazo la kutambuliwa kwa ushindi wake, Biden alisema hatua hiyo, inadhihirisha kwamba demkorasia ya Marekani imeshinda. **DW**

## Somalia yavunja uhusiano na Kenya

**Khartoum,** SUDAN

SERIKALI ya Somalia, imekatiza uhusiano wa kidiplomasia na nchi jirani ya Kenya.

Nchi hiyo imewaita nyumbani wanadiplomasia wake wote kutoka Nairobi na kuwapa wanadiplomasia wa Kenya muda wa siku saba, kuondoka nchini humo.

Tangazo hilo limetolewa na Waziri wa Habari, Osman Abukar Dubbe katika chombo cha habari cha kitaifa.

"Serikali ya Somali, kulingana uhuru wake iliyohakikishiwa na sheria ya kimataifa, inatekeleza wajibu kwa mujibu wa katiba ili kulinda utaifa, umoja na ustawi wa nchi imeamua kukatiza uhusiano wake wa kidiplomasia na serikali ya Kenya," alisema.

Hatua hiyo inakuja baada ya Somalia kuwasilisha barua ya malalamiko dhidi ya Kenya kwa Waziri Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, ambaye ni Mwenyekiti wa Viongozi wa Nchi Wanachama wa Muungano wa Maendeleo Afrika Mashariki na pembe ya Afrika **(IGAD).**

# IBRAHIMOVIC ATOA WITO UBINGWA MILAN




**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amesisitiza vinara wa Ligi Kuu Italia, Serie A, AC Milan wanahitaji "nguvu za ziada" kunyanyua taji la ligi hiyo kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10.

Ibrahimovic alikuwa mfungaji bora wa Milan, akifunga mabao 14 wakati 'Rossoneri' hao walipobeba kwa mara ya mwisho taji hilo mwaka 2011 ambalo lilikuwa la 18 kwenye historia ya klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu, akifunga mabao 10 katika mechi sita za ligi na kukifanya kikosi hicho cha kocha, Stefano Pioli kikiwa hakijafungwa hadi sasa na kinaongoza kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya wapizani wao Inter Milan baada ya mechi 11.

Mabingwa watetezi Juventus wametawala Serie A kwa zaidi ya muongo mmoja, lakini Ibrahimovic ana imani kubwa kwamba, Milan wanaweza kukipiku 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin na kutwaa taji hilo kwa mara ya 10 mfululizo.

"Timu inatakiwa kujituma na kuwa na hamasa kubwa ya kulitwaa taji la Scudetto, bado tuna safari ndefu ya kwenda," alisema Ibrahimovic, ambaye amerudi kwenye mazoezi kuelekea mchezo wa leo, Jumatano dhidi ya Genoa baada ya kupona majeraha ya misuli.

"Timu ina njaa na ipo tayari, tunataka zaidi na zaidi. "Nafikiri tunatakiwa kuwa na morali sawa pamoja na wachezaji wenzangu, mara zote nataka kufanya mazoezi kwa sababu najihisi kuwa bora zaidi."




# Ronaldo: Ni heshima kubwa kujumuishwa na Pele, Messi

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo amesema amepewa "heshima kubwa" kujumuishwa kwenye kikosi cha wachezaji 11 bora wa wakati wote na Jarida la France Football.

Jarida hilo la Ufaransa, Jumatatu lilitoa orodha ya kikosi bora cha wachezaji 11 cha wakati wote, huku nyota huyo wa Juventus, Ronaldo akitajwa pamoja na nahodha wa Barcelona, Lionel Messi, Pele na Diego Maradona ambaye alifariki mwezi uliopita.

Gwiji wa Brazil, Ronaldo de Lima, nahodha wa zamani wa AC Milan, Paolo Maldini, Xavi, gwiji wa Bayern Munich, Franz Beckenbauer, Lothar Matthaus, Cafu na golikipa Lev Yashin walikamilisha kikosi hicho cha wachezaji 11.

Baada ya kutoka kwa orodha hiyo, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Nimepewa heshima kubwa sana kuwa sehemu ya kikosi cha wachezaji 11 wa wakati wote na Jarida la France Football."

"Ni ndoto ya kuvutia sana... wote wanastahili heshima yangu na kwa hakika kabisa najisikia fahari kuwa mmoja wa wachezaji wa aina yake. Asanteni!"

Ronaldo ni mfungaji wa wakati wote wa Real Madrid akiwa ameshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, matatu ya Ligi Kuu England, taji la Euro 2016, mawili ya Serie A na kwenye LaLiga.

Ronaldo alisherehekea kufikisha mechi 100 kwa Juventus mwishoni mwa wiki wakati akifunga mabao mawili katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Genoa kwenye Serie A.

# Lampard bado hana imani kikosi Chelsea

**LONDON,** England

FRANK Lampard amekataa tena madai kwamba, Chelsea ina kikosi imara zaidi kwenye Ligi Kuu England kwa sababu kikosi chake bado hakijashinda chochote.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, alikitaja kikosi hicho cha 'Blues' kuwa kina nafasi kubwa ya kulitwaa taji hilo mapema mwezi huu, baada ya kutumia zaidi ya pauni milioni 200 kwenye usajili.

Chelsea walikuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo na walikuwa hawajapoteza mechi 13 katika mashindano yote, lakini wakafungwa na Everton bao 1-0 na kuwavuta hadi nafasi ya tano, wakipitwa pointi tatu kutoka kileleni.

Na Lampard hakubali kwamba yeye ana kikosi imara zaidi kwenye ligi hiyo msimu huu.

"Sioni kabisa hilo. Sikishushi kikosi changu kwa kusema hivyo," alisema.

"Baadhi ya watu wanasema kwamba tuna kikosi imara zaidi na ndio hao hao walikuwa wanasema hatuko vizuri wakati tulipotoka sare ya mabao 3-3 na West Brom na sare dhidi ya Southampton. "Mawimbi yamepinduka haraka. mjadala huo si muhimu kwa sababu ni kile tu tunachokifanya uwanjani ndio kinamaana.



HABARI MICHEZO

# Ferguson amlilia Houllier

**LONDON,** England

ALEX Ferguson ametuma salamu za rambirambi kwa kifo cha kocha wa zamani wa Liverpool, Gerard Houllier na kumuita "mtu wa kweli" baada ya kufariki dunia akiwa na umri wa miaka 73.

Houllier aliiongoza Liverpool kwa misimu sita hadi mwaka 2004 na alishinda mataji matano na klabu hiyo, ikiwamo mataji matatu kwa msimu mmoja wa 2000-01, pamoja na Ngao ya Jamii mwaka 2001.

Mfaransa huyo alikuwa mshindani wa gwiji wa Manchester United, Ferguson wakati wa kipindi chake akiwa pale Anfield, na wawili hao walikuwa na urafiki mzuri nje ya dimba.

Akizungumza Jumatatu baada ya kifo cha Houllier, siku moja baada ya kufanyiwa operesheni ya moyo, Ferguson aliiambia tovuti ya United: "Habari hizi zimekuja kwa mshituko mkubwa sana kwangu asubuhi hii (juzi).

"Gerard Houllier alikuwa bado kijana mdogo kwa umri wa miaka 73. Gerard alikuwa rafiki wa kweli kipindi chake akiwa pale Liverpool.

"Tuliendelea kuwa mafariki wazuri baada ya yeye kuondoka na mara zote tulikuwa tukiwasiliana.

"Alikuwa na ujuzi mkubwa zaidi wa soka kwa kipindi chote ambacho alikuwa kocha.






# RAIOLA AIPOZA MAN UNITED KWA POGBA

**TURIN,** Italia

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amebainisha kwamba, kiungo huyo ataondoka Manchester United, lakini hatarajii kwamba ataondoka wakati wa dirisha dogo la usajili Januari.

Raiola alibainisha kwenye mahojiano na Tuttosport baada ya United kutolewa na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa wiki iliyopita kwamba, muda wa Mfaransa huyo kukaa katika klabu hiyo "umefikia mwisho".

Pia alisisitiza mteja wake huyo hana furaha kuendelea kukaa pale United na yupo tayari kurudi Juventus, ambako alishinda mataji manne ya Serie A kabla ya kurudi Old Trafford.

Akizungumza kwenye tuzo za Golden Boy 2020 Jumatatu, Raiola alifafanua kauli yake hiyo aliyoitoa kuhusu Pogba.

"Nimeelezea maoni yangu na nilichosema kipo wazi kabisa," alisema Raiola.

"Nilikuwa nazungumzia kuhusu kipindi cha majira ya joto. Wachezaji wakubwa huwa hawaondoki Januari. Ngoja tuangalie nini kitatokea kipindi cha majira ya joto.

"Kwa bahati mbaya nchini England wapo makini sana linapokuja suala la Pogba. Lakini naamini atakuwa na siku nzuri zaidi siku zijazo."

Pogba, ambaye mkataba wake wa sasa na United unamalizika mwaka 2022, pia amekuwa akiwaniwa na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris Saint-Germain na Real Madrid.

# *Juventus kumpa Dybala unahodha akisaini*

**TURIN,** Italia

PAULO Dybala amepewa ofa nono ya kusaini mkataba mpya na kuwa nahodha wa Juventus kama atakubali kubaki klabuni hapo, Rais Andrea Agnelli amedai.

Dybala mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022 na alizungumza hivi karibuni uvumi wa kuhusu majaliwa yake unamweka kwenye wakati mgumu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alisema, "mambo mengi ambayo yamekuwa yakisemwa si ya kweli" na wakala wake "hakuitwa na klabu", akiongeza mapenzi anayopewa na mashabiki wa Juve yanaweza kubadilika.

Na bosi huyo wa 'Bianconeri', Agnelli aliibuka Jumatatu na kuelezea mipango yao kwa Dybala hapo Turin.

"Nimesikiliza maneno yake kuhusu mapenzi yake kwa Juventus," alisema Agnelli wakati Dybala akipokea tuzo ya Golden Boy iliyotolewa na gazeti la Tuttosport.


"Kwenye mipango yetu, yeye ndio nahodha ajaye, hata kama ameshavaa kitambaa hicho mara kadhaa.

"Naelewa kwamba, amepokea ofa kutoka klabu kadhaa ambayo itamfanya kuwa mmoja wa wachezaji 20 wanaolipwa zaidi Ulaya.

"Tunasubiria kwa utulivu mkubwa. Na hiyo inaonyesha wazi namna gani hata sisi tulivyo na mapenzi kwake."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: ARTETA NI KOCHA SAHIHI ARSENAL

●●● Yeye ni mmoja wa makocha bora, unajua katika duniani hii, watu wanafikiri hakuna muda...

**LONDON,** England

PEP Guardiola anaamini Mikel Arteta ni mtu sahihi kuiongoza Arsenal licha ya kuwa na mwanzo mbaya wa msimu wa 2020-21 kwenye Ligi Kuu England.

**Arsenal ilifungwa na Burnley pale katika dimba la Emirates Jumapili, kikiwa ni kichapo cha nne mfululizo nyumbani kwenye ligi na wakiweka rekodi ya kuwa na mwanzo mbaya zaidi tangu mwaka 1959.**

'Washikabunduki' hao wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi, wakipitwa pointi 10 kutoka nne bora na wakiwa juu kwa pointi tano tu kutoka mstari wa kushuka daraja.

Kudidimia chini kwa Arteta, msaidizi wa zamani wa Guardiola pale Manchester City, kumekuwa kwa rahisi sana baada ya Arsenal kumaliza msimu uliopita kwa mafanikio ya kubeba taji la FA.

Sasa presha imekuwa juu kuhusu kocha huyo, ambaye ameshindwa kupata kilicho bora kabisa kutoka kwa nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang.

Straika huyo ambaye alisaini mkataba mnono kabla ya kuanza kwa msimu huu, amefunga mara mbili tu kwenye ligi, huku bao la kujifunga dhidi ya Burnley likiamua matokeo.

Wakati Aubameyang akikabiliwa na wakati mgumu, Arsenal imefunga mabao 10 tu ya ligi katika mechi 12, yakiwa machache zaidi kwa kipindi cha miaka 39. Lakini Guardiola bado anaendelea kumuunga mkono Arteta.

"Arsenal haina kocha mwingine wa kuiongoza klabu hiyo kwa ubora zaidi, miaka inayokuja zaidi ya yeye," alisema bosi huyo wa City akiwaambia waandishi wa habari.

"Yeye ni mmoja wa makocha bora zaidi ambao nimewahi kufanya nao kazi, bila shaka yoyote naweza kuona ubora wake na namna anavyojitoa na mapenzi yake kwa klabu.

"Kwa uhakika kabisa atabadilisha mambo pale kama ambavyo kila mmoja anatarajia na vile anavyotaka.

"Wakati mwingine klabu inapofanya vibaya, unahitajika muda wa kusubiri. Unajua katika duniani hii watu wanafikiri hakuna muda wa kusubiri."

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMUUZA XHAKA

ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wake, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28 raia wa Uswisi, baada ya nyota huyo kutolewa nje kwa kadi nyekundu kutokana na kumkaba kwenye koo, Ashley Westwood wa Burnley wakati 'Washikabunduki' hao wakichezea kichapo Jumapili. ***(Mail)***

### UNITED HOI KWA COMAN

MIPANGO ya Manchester United kumsajili winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman, imepatwa na pigo baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo ya Ujerumani, Karl-Heinz Rummenigge, kusema nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ufaransa, hauzwi. ***(Kicker, via Sun)***

### BALE KURUDI REAL MADRID

WINGA wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, anatarajia atafanya vema zaidi Real Madrid, baada ya kuwa Tottenham Hotspur kwa mkopo. ***(AS)***

### WILLIAMS KUTUA S'AMPTON

KLABU ya Southampton imepania kumsajili kwa mkopo mlinzi wa kushoto wa Manchester United, Brandon Williams, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Telegraph)***

### MARCELO KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inaweza kumsajili kiungo wa kati wa Lyon, Marcelo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Brazil, kwa uhamisho huru msimu ujao. ***(Sun)***

### ERIKSEN HAITAKI TENA EPL

KIUNGO wa Inter Milan, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, hana mpango wa kurudi tena Ligi Kuu England na hajakubali kuhamia Paris St-Germain. ***(Star)***

### SALIBA KUBAKI ENGLAND

MLINZI wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, yuko tayari kucheza kwingine kokote England kwa mkopo, badala ya kurejea Ufaransa Januari. ***(The Athletic)***

### DYBALA AUMBULIWA JUVE

RAIS wa Juventus, Andrea Agnelli amesema klabu hiyo imempatia ofa ya kurefusha mkataba mshambuliaji wake raia wa Argentina, Paulo Dybala, baada ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27- kudai hajapewa mkataba wowote. ***(Tuttosport via Football Italia)***

### DEENEY AMFUNDA ARTETA

MSHAMBULIAJI wa Watford, Troy Deeney, amesema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta lazima afanye mkutano wa dharura na wachezaji baada ya klabu hiyo kupoteza kwa Burnley wikendi iliyopita. ***(Talksport)***

### EVERTON KUMBAKIZA SMALL

EVERTON ina imani ya mlinzi wake wa kushoto, Thierry Small kubaki klabuni hapo, licha ya dogo huyo mwenye umri wa miaka 16, kunyatiwa na Arsenal, Bayern Munich na Juventus. ***(Liverpool Echo)***

## Mauti ilivyomkuta mwigizaji Mzee Jengua

**Na Adam Fungamwango**

MWIGIZAJI mkongwe na maarufu nchini, Mohamed Fungafunga maarufu 'Mzee Jengua' kwa jina la kisanii, amefariki dunia Mkuranga mkoani Pwani jana.

Kwa mujibu wa mke wa marehemu aliyejitambuliwa kwa jina la Maua Ally, marehemu amefariki dunia nyumbani kwa mtoto wake mkubwa, Mkuranga alikokuwa akiuguzwa ugonjwa wa shinikizo la damu.

"Alikuwa anasumbuliwa na presha, tulikuwa Mkuranga kwa mtoto wake mkubwa kwa ajili ya kumuuguza, lakini leo (jana) asubuhi hali yake ikawa mbaya, akafariki dunia hapa hapa nyumbani," alisema Maua huku akilia.

Chama cha Waigizaji mkoani Dar es Salaam (TDFAA) kupitia kwa Katibu wake, Doricy Kente, nacho kimeeleza kupokea taarifa za msiba wa mwigizaji huyo aliyejizolea sifa na umaarufu mkubwa kwa kuigiza kama baba au mume mwenye misimamo mikali na kusimamia kile alichokiamini na si vinginevyo.

Umaarufu wa mwigizaji huyo ulianza mwanzoni mwa miaka ya 2000 kwenye michezo ya kuigiza iliyokuwa ikirushwa na Televisheni ya ITV, na mchezo uliomfanya kila mtu amfahamu na kuheshimu kipaji chake ni 'Kidedea' ambao ulitayarishwa na Kikundi cha Chemchem Arts Group, akiigiza kama mzee mmoja 'mnoko' mkali na hiyo ilikuwa ndiyo kama nembo yake kwenye michezo mingi baadaye, akipata tenda ya kucheza filamu nyingi kuanzia mwaka 2010 na kuendelea hadi kifo chake.



Filamu kama "Handsome wa Kijiji na 'Keshinde' pia zilimpatia umaarufu mkubwa.

Kwa mujibu wa mkewe, msiba wa mzee Jengua uko Mkuranga, nyumbani kwa mtoto wake, lakini mazishi ya nguli huyo yanatarajiwa kufanyika nyumbani kwake Mburahati, kwenye makaburi ya Mburahati jijini Dar es Salaam.

# FIFA YAMFUNGULIA KICHUYA KUKIPIGA RASMI NAMUNGO

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikipambana kuomba mapitio upya ya hukumu waliyopewa ya kulipa dola za Marekani 127,000 (Sh. milioni 292 za Tanzania), Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), limetoa baraka zake kwa Namungo FC kuendelea kumtumia winga Shiza Kichuya, imeelezwa.

**Kichuya alifungiwa na FIFA kucheza kwa muda wa miezi sita, huku Simba ikipigwa faini hiyo kutokana na kumtumia mchezaji huyo kinyume cha taratibu za usajili, kwa maelezo kuwa wakati anawatumikia mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, bado alikuwa na mkataba na Klabu ya Pharco ya Misri.**

Lakini Katibu Mkuu wa Namungo FC, Suleiman Ali, amesema tayari wamepokea barua kutoka FIFA inayowataka kuendelea kumtumia Kichuya katika michezo yote ya timu hiyo kwa sababu Simba wamepeleka malalamiko yao katika shirikisho hilo wakiomba kupitia upya kwa shauri hilo.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, baada ya kumalizika kwa mechi yao dhidi ya Azam FC kwa kulazimisha sare ya mabao 2-2, iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, katibu huyo alisema walipokea barua kutoka FIFA kuhusu utaratibu wa nyota huyo kutakiwa kucheza hadi hapo shauri la Simba litaposikilizwa.

Alisema Kichuya ataendelea kuitumikia timu yao kwa sababu Simba imekata rufani ya kuomba FIFA kufanya mapitio upya ya shauri linalohusu wao na mchezaji huyo ambaye anaichezea Namungo.

"Kuna taarifa tumeipokea kuhusu Kichuya kwamba anaweza kucheza hadi hapo FIFA itakapopitia shauri hili upya, kwa hatua hiyo tunaendelea kumtumia mchezaji huyo kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi, chini ya Kocha Mkuu, Hemed Morocco," alisema Suleiman.

Alisema kulingana na barua hiyo watamtumia nyota huyo katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa muda ambao shauri hilo linaendelea kupitiwa.

"Basi kama itabainika kwamba Kichuya na Simba wana makosa, adhabu hiyo itaanzia hapo, kwa nyota wetu huyo kufungiwa miezi sita na 'Wekundu wa Msimbazi' hao kulipa dola 127,000," alisema katibu huyo.

Kichuya alisajiliwa na Simba kwenye usajili wa dirisha dogo Januari mwaka huu, akitokea Klabu ya Pharco ya Misri ambayo inadai kwamba alikuwa na mkataba wa miaka miwili na aliitumikia kwa mwaka mmoja, jambo lililowafanya kupeleka malalamiko hayo FIFA.




Wanafunzi wa Shule ya Awali ya St. Mary's Mbezi Makonde jijini Dar es Salaam, wakionyesha umahiri wao wa kuimba na kucheza nyimbo mbalimbali wakati wa mahafali ya elimu ya awali shuleni hapo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Lwandamina kwenda sokoni kuisuka Azam FC*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, George Lwandamina, amekiri kuona upungufu ndani ya timu hiyo na kueleza dhamira yake ya kutaka kuiboresha baada ya usajili wa dirisha dogo kufunguliwa rasmi jana.

Lwandamina alitoa kauli hiyo katika Uwanja wa Azam Complex juzi, baada ya kumalizika kwa mechi yao dhidi ya Namungo FC waliyotoshana nguvu kwa sare ya mabao 2-2.

Alisema anahitaji kukaa na uongozi wa klabu hiyo kueleza udhaifu wa kikosi chake, na kwamba kutokana na ushindani uliopo Ligi Kuu Tanzania Bara, anapaswa kueleza mahitaji yake ili kufanya vizuri katika ligi hiyo.

"Usajili ni kwa ajili ya timu kubwa na sisi pia lazima tufanye usajili kutokana na mapendekezo yangu ambayo nitayatoa nitakapokutana na viongozi kuwaeleza ni wapi na mchezaji gani ambaye atatusaidia kufikia malengo yanayotarajiwa," alisema Lwandamina.

Alisema upungufu aliouona ni ule ule katika michezo yote miwili dhidi ya Namungo na Gwambina FC ambao alikuwa jukwaani akishuhudia.

"Timu ni nzuri, lakini kuna upungufu ambao unatakiwa kufanyiwa kazi kipindi cha usajili, nitaweka wazi kwa uongozi kwa kuwaeleza mahitaji na aina gani na nafasi ipi ambayo ninatakiwa kuboresha," alisema Lwandamina.

Akizungumzia mechi hiyo dhidi ya Namungo, alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa pande zote mbili, kwa wapinzani wao kutumia makosa yao kusawazisha mabao mawili baada ya wao kuwa mbele.

"Kwa matokeo hayo, bado hatujakata tamaa kwa suala la ubingwa, nina imani ni kujipanga na wachezaji kujitolea katika kila mechi kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mechi zote zilizopo mbele yetu," alisema.

Azam ambayo imeshuka dimbani mara 15 hadi sasa, ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 28, moja nyuma ya Simba iliyopo nafasi ya pili baada ya mechi 13, huku Yanga iliyocheza mechi sawa na 'Wanalambalamba' hao, ikiwa kileleni na alama zake 37.

# Michezo

Jumatano Desemba 16, 2020

Nipashe




Mauti ilivyomkuta mwigizaji Jengua UKURASA 23

JAMBO LAO LEO...



Mastraika wa Simba; kutoka kushoto, Chris Mugalu na Meddie Kagere pamoja na kiungo mnyumbulifu Clatous Chama, ambao wanaweza kuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa KMC FC, timu hizo zitakapokutana kwenye mechi ya Ligi Kuu katika Uwanja wa Taifa leo. **PICHA: MAKTABA**

## Kaze akabidhi majembe Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU kukiwa na taarifa ya Yanga kuwania saini ya kiungo wa Plateau United ya Nigeria, Isah Ndala, pamoja na washambuliaji wawili wanaocheza soka nchini, Adam Adam wa JKT Tanzania na Mghana anayekipiga katika kikosi cha Namungo FC, Steven Sey, uongozi wa klabu hiyo umesema tayari umepokea na unafanyia kazi mapendekezo ya Kocha Mkuu, Cedric Kaze.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Yanga, Hersi Said, alisema wamepokea mapendekezo kutoka kwa kocha wao mkuu, Kaze kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea mipango yao waliyojiwekea msimu huu. Alisema maingizo mapya yanakuja na wanaendelea kufanya mazungumzo na baadhi ya wachezaji mbalimbali ili kutekeleza mapendekezo hayo ya kocha.

"Kwa sasa tunaendelea na utaratibu huo wa kusajili na wachezaji ambao watatolewa kwa mkopo kutokana na mapendekezo ya kocha, tukimaliza utaratibu huo tutaweka wazi tuliowasajili na wale wa kutolewa kwa mkopo," alisema Hersi.

Hersi alisema Said Ntibazonkiza amekuwa wa kwanza katika usajili huo na kwa mujibu wa Kaze nyota huyo ataanza kucheza ligi hiyo, katika mechi yao dhidi ya Dodoma jiji FC Jumamosi wiki hii.

Wachezaji ambao Nipashe limedokezwa kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo kuwa huenda wakatolewa kwa mkopo ni Abdulaziz Makame, Juma Mahadhi, Abdallah Shaibu 'Ninja', Adeyum Salehe, Waziri Junior na Paul Godfrey.

# Simba, Yanga kukinukisha Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

### ●●● Wekundu wa Msimbazi wakubali wakitaka ratiba Ligi ya Mabingwa imulikwe, kuivaa KMC leo huku...

WAKATI Simba wakishuka dimbani leo kuikaribisha KMC FC kwenye kinyang'anyiro cha Ligi Kuu Tanzania Bara, mabingwa watetezi hao pamoja na watani wao wa jadi, Yanga, wamekubali kwenda visiwani Zanzibar kushiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi, imeelezwa.

**Simba iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara 13 na kujikusanyia pointi 29, moja mbele ya Azam FC iliyopo nafasi ya tatu kutokana na kucheza mechi 15 sawa na Yanga ambayo ipo kileleni ikiwa na alama 37, itahitaji ushindi leo, ili kuendelea kuwafukuzia watani zao kileleni.**

Hata hivyo, baada ya mchezo huo wa leo, Simba haitashuka tena dimbani kucheza mechi ya Ligi Kuu, na badala yake itaingia kwenye maandalizi ya safari ya kwenda kuivaa Platinum ya Zimbabwe kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tayari Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, ameeleza lengo lao ni kushinda mechi hiyo ya leo na nyingine, ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa huo, lakini hawataki kupoteza lolote kuelekea mchezo wao wa raundi ya kwanza dhidi ya Platinum utakaopigwa Desemba 23, mwaka huu.

Kuhusu michuano ya Kombe la Mapinduzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Omar Hassan Omar, alisema jumla ya timu tisa zitashiriki michuano hiyo, tano zikiwa ni kutoka Tanzania Bara na nne za visiwani Zanzibar.

Mbali na Simba na Yanga, Omar alizitaja timu zingine zitakazoshiriki kutoka Tanzania Bara kuwa ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Mtibwa Sugar, Azam FC na Namungo FC, huku kwa upande wa visiwani Zanzibar zikiwa ni timu mbili za Ligi Kuu Zanzibar; Mlandege na Malindi pamoja na mbili kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba ambazo ni Jamhuri FC na Chipukizi.

Alisema tayari Yanga imethibitisha kushiriki michuano hiyo inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi visiwani Zanzibar kati ya Januari Mosi ama 3, mwakani, lakini kwa upande wa Simba na Namungo licha ya kukubali, zimesema ushiriki wao utategemeana na ratiba ya Ligi Kuu Bara na ile ya mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika itakavyokuwa.

Simba inaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Namungo pia ikiwa na kibarua cha kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho.

Aidha, katibu huyo alitaja kamati itakayosimamia mashindano hayo ambapo Mwenyekiti atakuwa ni Khamis Abdallah Said, Katibu ni Aiman Duwe na Naibu Katibu akimtangaza kuwa ni Suleiman Pandu.

Kwa upande wa Wajumbe wa Kamati ya Mashindano ya Kombe la Mapinduzi, aliwataja kuwa ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu Wizara ya Michezo Muungano, Dk. Hassan Abbas, Mratibu wa Shughuli za Serikali (SMZ), Issa Mlingoti na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo nchini, Omar Singo.

Wajumbe Wengine ni Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Neema Msika, Ambar Sharif, Meneja wa Uwanja wa Amaan na Mau, Abdulhamin Mohamed Juma, Ofisa Mdhamini Wizara ya Habari, Fatma Hamad Rajab, Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, Makamu wa Rais wa ZFF, Salum Ubwa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Zanzibar, Chande Omar na Juma Mmanga.

"Mbali na mashindano hayo ya wakubwa, pia kutakuwa na michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa upande wa timu za vijana pamoja na wanawake kwa mpira wa miguu," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wadau wa michezo Zanzibar kushirikiana kwa pamoja katika suala hilo la michezo ili kufikia lengo la serikali la kuendelea kuinua sekta hiyo visiwani Zanzibar.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042